# GUNDUA ULIMWENGU WAKO WA KAZI

MADA YA

# 3

***Alama ya Chapisho***

Februari 2022

Programu ya 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' linaweza kuwa huru kutumika, kwa vile chanzo kimetajwa.

***Ilianzishwa na:*** Wil Bom, VSO, mradi wa Vijana na Ajira, Zanzibar, Tanzania

***Kwa ushirikiano na:*** Walimu na wakufunzi wasaidizi wa makundi manne ya Mafunzo ya Ufundi (Amali), Unguja na Pemba; Sophie Oonk wa Randstad Uholanzi ambaye aliendeleza mada ya 5 'Gundua biashara yako'; Kitty den Boogert, rafiki na mwenzangu wa zamani, ambaye aliangalia toleo la mwisho.

***Kwa kuzingatia:*** Warsha (ya mafunzo) ya maendeleo ya kazi, iliyotolewa wakati wa maonesho ya Zanzi Job ya mwaka 2015 na 2016.

Utangulizi wa VSO-ICS juu ya uajiri na ujuzi wa maendeleo ya kazi katika mwaka 2015 na warsha (za mafunzo) zilizotolewa na Watu wenye Kujitolea wa Huduma za Wananchi, Kimataifa.

Mwongozo wa mafunzo, Elimu ya Ujasiriamali na Mafunzo ya EET, Kuboresha Uwezeshaji wa Kiujasiriamali, Moduli ya 1 na 2, VETA, 2014 – 2008.

Maendeleo ya programu kwa mwongozo wa kazi katika mafunzo ya ufundi na CINOP, Uholanzi. www.cinop.nl

Loopbaanmagazijn (Hifadhi ya kazi), ilianzishwa na Claudine Hogenboom, mradi wa Mwongozo wa Kazi kwa mafunzo ya ufundi, Uholanzi. http://www.expertisepuntlob.nl/

Het lespakket netwerken (Mtandao wa Mtaala), ilianzishwa na La Red B.V., Uholanzi. http://lared.nl/

***Tafsiri ya Kiswahili:*** Abdalla Baruan, Dar es Salaam, abbybaruan@gmail.com
Abraham Mtongole, Dodoma, abmtongole@gmail.com
Yahya Abdu, Pemba, Tafsiri ya kiswahili na uhakiki wa toleo la mwisho, yahyarashid@live.com

***Ubunifu:*** Katie Wolgemuth, VSO Dar es Salaam na wanafunzi wa GLU, Grafisch Lyceum Utrecht

***Ilichapishwa na:*** VSO Tanzania, S.L.P 6297, Dar es Salaam Tanzania

***Eneo:*** Ploti na. 997 Msasani, Barabara ya Chole, Dar es Salaam Tanzania

***Simu:*** (+255) 222600072 au (+255) 222600087


***Barua pepe:*** vsotanzania@vsoint.org

***Tovuti:*** www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet



# MAENDELEO YA KAZI NAMNA YA KUWAONGOZA VIJANA KWENYE MAFUNZO YA UFUNDI NA AJIRA AU AJIRA BINAFSI?

## MADA YA 3 GUNDUA ULIMWENGU WAKO WA KAZI



# YALIYOMO

Kitabu hiki 'Gundua ulimwengu wako wa kazi' ina vifaa kwa ajili ya mada ya 3 ya programu kwenye Maendeleo ya Kazi. Kwanza, unakuta utangulizi wa jumla kwenye programu na namna ya kuandaa mafunzo. Hii inafuatiwa na maelezo mahsusi ya jumla ya mazoezi ya mada ya 3, maelekezo tofauti kwa kila zoezi na karatasi za mazoezi.


| | |
|---|---|
| Utangulizi wa jumla Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi naa jira au ajira binafsi? | 6 - 11 |
| Mada ya 3 na maelezo ya jumla ya mazoezi 'Gundua ulimwengu wako wa kazi' | 12 - 15 |
| Mada ya 3: mazoezi 3.1 - 3.24 | 16 - 63 |
| Karatasi za mazoezi | 64 - 75 |


Vichwa vya vitabu vyote sita vya programu ya Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi? ni:

1 Gundua kipaji chako
2 Gundua shauku yako
3 Gundua ulimwengu wako wa kazi
4 Gundua mtandao wako
5 Gundua biashara yako
6 Mpango kazi wako na kuomba kazi

Uwasilishaji wa pawapointi na karatasi za mazoezi zinaweza kupakuliwa kutoka www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet

# UTANGULIZI WA JUMLA

# MAENDELEO YA KAZI: NAMNA YA KUWAONGOZA VIJANA KWENYE MAFUNZO YA UFUNDI NA AJIRA AU AJIRA BINAFSI?


**Mradi wa VNA na programu ya 'Ulimwengu Wangu wa Kazi'**
Vijana na Ajira (VNA), mradi wa Vijana na Ajira ni moja ya miradi ya VSO, Volunteer Services Oversee (Huduma za Kujitolea, Ng'ambo) kwa ushirikiano na RGZ, (Revolutionary Government of Zanzibar/Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar). Moja ya vipengele vya mradi wa VNA ni programu ya 'Ulimwengu Wangu wa Kazi' (UWwK). Programu ya UWwK hutaka kuimarisha nafasi ya kijamii na kiuchumi ya vijana ndani ya Zanzibar kwa kuendeleza ustadi mbalimbali wanaouhitaji kwa ajili ya ajira, ajira binafsi au ujasiriamali. Kwa kusudio hilo, viunganishi madhubuti zaidi baina ya sekta binafsi na mafunzo ya ufundi ni muhimu. Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi (Amali) (MMA), NACTE (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi), Vituo vyote vya Mafunzo ya Ufundi (Amali) na Taasisi za Zanzibar zinahusishwa kama washirika katika programu hii ya UWwk. Wana majukumu makubwa katika kuwawezesha vijana pamoja na ujuzi muhimu kuingia katika soko la ajira.

Programu ya UWwK imezalisha sanduku la zana kwa masomo mawili ya msingi: Mafunzo na Elimu ya Kuzingatia Umahiri na Maendeleo ya Kazi. Unaweza kupata sanduku zima la zana kwenye mtandao: www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet

**Maendeleo ya Kazi**
Programu ya 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' ikiwemo uchaguzi mpana wa mazoezi ya darasani ambayo husaidia wanafunzi, watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi kupata kuonekana zaidi katika mazingira ya kazi. Kwa kufanya kazi, wote, wale wa ndani ya darasa na nje katika mazingira halisi, vijana hupata habari za hapo kwa hapo kuhusu ulimwengu wa kazi, hufanya kwa vitendo ujuzi tofauti wanaouhitaji kwa ajili ya maendeleo yao ya kazi na hubadilishana uzoefu kwa kila mmoja kati yao. Vipindi vitabuniwa na kutolewa na VMA (Vituo vya Mafunzo ya Amali), Taasisi za Ufundi, Skuli za Sekondari na mashirika mengine ya kiserikali na yasio ya kiserikali, kawaida ni kwa mchango wa wafanya biashara wa ndani (wenyeji). Waajiri na kiongozi (meneja) wa rasilimali watu anaweza kuwa msaada kwa kuwezesha safari za kimasomo, kwa kuwa mkufunzi mgeni wa ndani ya madarasa au kwa kutoa mafunzo ya viwandani.

**Programu ya Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?**
Programu ya Maendeleo ya Kazi huwawezesha walimu wa skuli za sekondari, wakufunzi wa taasisi za mafunzo ya ufundi, kampuni, taasisi zisizo za kirerikali, wizara ya Kazi, Ajira, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Amali) kuchagua mazoezi ambayo yanafaa kwa mahitaji na kiwango cha makundi yao ya vijana.

Programu hailengi kwa vijana kufanyia kazi kwa kujitegemea, bila mwongozo wowote. Bila shaka, washiriki hupata kazi au kazi fulani ya kufanya mmoja mmoja, lakini kwa jumla, hii ni programu ambayo inahitaji mwingiliano, ushirikiano katika makundi na mrejesho. Haiwezi kufuatwa bila mwongozo. Hakikisha unatoa daftari ambalo washiriki wanaweza kuandika na kuhifadhi matokeo na maendeleo yao. Kwenye gamba la daftari, unaweza kuweka mwelekeo wa kazi au washiriki wanaweza kubuni ukurasa wao wa mbele. Walimu na wakufunzi wanahitaji kujiandaa vizuri, na inapendekezwa kwamba mwanzo watafakari maendeleo yao wenyewe ya kazi. Kwa njia hii, walimu na wakufunzi pia ni mfano wa kuigwa katika kuendesha kazi yao wenyewe kiundani.




**Mahiri sita za kazi na dira ya kazi**
Programu 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' imeundwa karibu na mahiri sita ambazo ni muhimu wakati unapotaka kuendeleza kazi yako:

1 Gundua kipaji chako: tafakuri kuhusu uwezo, kupitia umahiri wako mwenyewe kwa heshma ya kazi yako;

2 Gundua shauku yako: tafakuri kuhusu hamasa, kupitia matakwa na maadili yako mwenyewe kwa heshima ya kazi yako;

3 Gundua ulimwengu wako wa kazi: utafutaji wa ajira, mwelekeo kuhusu maadili na umahiri wako kulinganisha na kinachohitajika katika hali ya kazi za kitaaluma;

4 Gundua mtandao wako: mtandao, kufanya na kudumisha mawasiliano ambayo ni muhimu kwa kazi yako;

5 Gundua biashara yako: utafutaji wa ajira binafsi, mwelekeo juu ya matarajio na umahiri wako kuanza biashara au kuendeleza kazi kama mjasiriamali;

6 Mpango kazi wako na kuomba kazi: udhibiti wa kazi, mipango inayohusiana na kazi na ufafanuzi binafsi wa nafasi kwa mchakato wako wa kujifunza na kazi.

Kila umahiri wa kazi umeshikamanishwa sambamba na swala la kazi na jumla ya mahiri sita zinawakilishwa kama usukani wa uendeshaji wa kazi. Unahitaji kuendesha hatua zako za kazi muda wote kutafuta mwelekeo sahihi. Katika maelezo ya kina ya kila moja ya mahiri sita za kazi, unaweza kupata ufafanuzi zaidi kuhusu umahiri unaouhitaji kufanya kwa vitendo, kuendeleza kazi.

**Namna ya kutumia programu kwenye Maendeleo ya Kazi?**
Kila umahiri wa kazi unaweza kufunzwa kwa kufanya mazoezi kadhaa. Mazoezi hutofautiana katika maudhui na katika mbinu pia. Hii ni nzuri, kwa kuwa kuna njia zaidi ya moja ya kujifunza umahiri wa kazi.

Mwanzoni mwa kila mada mpya, utakuta maelezo ya jumla ya mazoezi yote ambayo ni ya mada maalum. Katika maelezo hayo ya jumla, kawaida unakuta: jina cha zoezi, lengo na muhtasari wa mbinu chochezi ambazo zinaweza kutumika katika zoezi hili. Kwa njia hii, unaweza kuangalia kwa haraka mazoezi yote na hii itakusaidia kufanya uchaguzi unaokufaa na kundi lako. Uchaguzi mzuri ni ule unaohusiana na maswala ya maendeleo ya kazi ambao wanafunzi, watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanao.

Baada ya kuchunguza maelezo ya jumla, unaweza kuvuta mazoezi uliyochangua. Yote kati yao yana muundo sawa. Kwa njia hii, unaweza kuona kwa urahisi namna ya kuandaa na kutoa zoezi kwa njia inayofaa.

Kwa kufanya uteuzi wako mwenyewe, walimu na wakufunzi wanaweza kubuni programu ya mafunzo. Unachagua mazoezi yale ambayo yanafaa kwa mtaala, ratiba ya vipindi vya kozi na kiwango cha wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi. Uchaguzi unaofanya pia hutegemea na maswali ambayo wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanayo kuhusu kazi yao.

Walimu na wakufunzi wanaweza pia kuchagua yale mazoezi wanayopenda kusomeshea. Baadhi ya mazoezi na mbinu zitakufaa zaidi kuliko nyengine. Vidokezo vinavyotolewa mwishoni mwa maelekezo, ni mapendekezo ili kuwezesha zoezi liwe vizuri iwezekanavyo, lakini jisikie huru kulifanya kwa njia tofauti unazodhani zitakufaa au vizuri zaidi kwa kundi lako.

Bila shaka, unaweza kuongeza mazoezi yako mwenyewe kwenye programu hii. Kwa njia hii, sanduku la zana litakua na kwa kubadilishana mazoezi na wengine, mwongozo wa kazi utatolewa kwa njia nzuri zaidi kwa vijana wa Zanzibar na Tanzania.



**Muundo sawa katika mazoezi yote**
Mazoezi yote yanaelezwa kwa kina zaidi, kufuata muundo huo huo. Hii itakusaidia kuandaa na kuwezesha mazoezi uliyoyachagua. Muundo ni:

**Lengo:** Ni lipi madhumuni ya zoezi? Matokeo gani yatakuwa yanatarajiwa. Kuangalia ufahamu, tabia, ujuzi na vitendo?

**Maandalizi:** Kama mwalimu/mkufunzi, nini cha kufanya katika maendeleo ya kazi kwa ajili ya kutoa zoezi kwa namna ya kuzingatia mchakato? Jinsi ya kuandaa darasa kuwapa washiriki wako eneo wanalohitaji ili kufanya mazoezi? Baadhi ya mazoezi yanahitaji eneo zaidi au mpangilio tofauti wa viti/meza.

**Maelezo:** Kama mwalimu/mkufunzi, nini unaweza kuwaambia wanafunzi/watafutaji wa kazi wako na wabunifu wa kazi kama ni utangulizi kwenye zoezi?

**Utendaji:** Ni nini wanafunzi watafutaji wa kazi na watoaji wa kazi watalazimika kufanya au kuonesha katika zoezi hilo? Hapa, unaweza kupata mlolongo wa hatua ambazo washiriki huchukua ili kukamilisha zoezi.

**Tafakuri:** Mwaswali gani unauliza mwishoni mwa zoezi (au baada ya hatua mahsusi wakati wa zoezi)?

**Dondoo:** Vitu ambavyo unahitaji kuwa na uelewa navyo wakati wa zoezi.

**Uchunguzi wa kina:** Nini kinaweza kufanywa zaidi kulipa zoezi (kwenda) kina zaidi au kuliunganisha na zoezi jengine?

**Karatasi za mazoezi:** Misaada ya kujifunza, malighafi na vifaa ambavyo vinaweza kutumika na wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi.

# MADA YA 3

**Gundua ulimwengu wako wa kazi**
Katika mada ya 3 utakuta mazoezi 24 kuhusu umahiri wa kazi 'Gundua ulimwengu wako wa kazi': utafutaji wa ajira.

Gundua ulimwengu wako wa kazi inamaanisha: chunguza mahitaji na maadili ya sasa na baadaye katika taaluma unayotaka. Wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi huendeleza ujuzi ili kutafuta ajira ambayo inaenda sambamba na maadili yao binafsi. Hujifunza namna ya kutafuta usawa kati ya viwango vilivyopo/maadili ya sehemu ya kazi na vipaji/maadili yao binafsi. Utafutaji wa ajira ni juu ya kupata ladha ya uhalisia ya ulimwengu wa kazi.

Katika maelezo ya jumla ya mada ya 3 unaweza kuwa na uelewa wa fursa za kazi na kazi katika familia yako mwenyewe na mzunguko wa watu unaowajua; kuchunguza kazi katika kampuni kwa kuandaa usaili au ziara za kimasomo na kutafakari kuhusu hayo; kugundua aina ya kampuni unayotaka kufanyia mafunzo yako ya viwandani; kutathmini kama una umahiri unaohitajika na makampuni.

Nambari ambayo zoezi hilo linaendana na idadi ya maelezo ya kina ya zoezi hilo na ya karatasi za zoezi. Karatasi za zoezi zinaweza kunakiliwa kwa urahisi kwa ajili ya vijana wako. Hakikisha unatoa daftari ambapo washiriki wanaweza kuandika matokeo yao na wanaweza kuhifadhi matokea na maendeleo yao. Kwenye gamba la daftari, unaweza kuweka dira ya kazi au washiriki wanaweza kubuni ukurasa wao wenyewe wa mbele.



# MAELEZO YA JUMLA YA MAZOEZI 'GUNDUA ULIMWENGU WAKO WA KAZI'

| Mazoezi 'Gundua ulimwengu wako wa kazi' | Lengo la zoezi | Mbinu shirikishi |
|---|---|---|
| **3.1**<br>**Je, familia yangu ina aina gani ya kazi?** | Vijana wagundue aina ya kazi za wanafamilia yao na kutambua ushawishi wa kazi za kawaida/biashara katika familia zao juu ya vipaji vyao, shauku na malengo ya kazi zao wenyewe. | Vijana watengeneze mchoro wa ukoo na fani zote au biashara ndogo za wanafamilia kwa miaka iliyopita (mama/baba, babu, kaka/dada, wajomba/shangazi na binamu). Baada ya kutengeneza mchoro wafanye tafakuri juu ya maswali kama: Unapenda nini kuhusiana na wanavyoendesha maisha? Je, hupendezwi na nini? Ni mabadiliko gani ungehitaji kufanya? Kwanini? |
| **3.2**<br>**Mahojiano na mwanafamilia** | Vijana wachunguze njia ambazo ndugu zao wamezitumia kupata kazi mpaka sasa. Wajifunze pia ni muhimu na inavutia kiasi gani kuwa na mazungumzo na mtu mwingine kuhusu fursa za ajira na kazi. | Vijana waandae maswali ya mahojiano na jamaa zao. Kama kazi ya nyumbani, wafanye mahojiano na kuandaa taarifa fupi juu ya uwasilishaji. Tafakari juu ya matokeo ya wengine kwenye makundi yao. |
| **3.3**<br>**Maswali yangu kwa mtaalamu** | Vijana waandae mahojiano na mtaalamu. Katika somo moja au zaidi, watafanya mahojiano haya na mtu kutoka tawi au sekta inayowavutia zaidi. | Kwanza kijana mmoja mmoja aandae orodha ya maswali sita. Washirikishane orodha hiyo katika makundi ya watu watatu na kila kikundi kiandae orodha ya mwisho yenye maswali yasiyozidi 10. Baada ya hapo waweke miadi na mtaalamu atakayehojiwa darasani na vikundi vidogo vidogo. |
| **3.4**<br>**Kutarajia ziara ya kimafunzo** | Vijana wachunguze matarajio yao kuhusu ziara: kutembelea kampuni, shirika au biashara ndogo. | Katika sanduku zuri lenye maneno 'tazama mbele' juu yake, matarajio ya washiriki yatakusanywa. Kwenye vipande vitatu (3) vidogo vya karatasi kila kijana aandike jina lake na tarajio lake moja juu ya karatasi. Washirikishane matarajio yao na kuweka karatasi katika sanduku. Baada ya ziara, sanduku litafunguliwa na watafanya zoezi 3.11 'Tazama nyuma'. |
| **3.5**<br>**Kama iwavyo kazini!** | Vijana wagundue ujuzi waliopata katika kazi zao zisizo rasmi na kuchunguza matarajio yao kuhusu ziara ya kutembelea kampuni. | Katika kundi la watu watatu washirikishane uzoefu wao wa kazi, kazi walizofanya. Wajadili uhalisia wa yale waliyojifunza/kufanywa hadi sasa kutokana na kazi zilizofanywa na kampuni watakayotembelea. Baada ya hapo wanaweza kuweka matarajio yao juu ziara hiyo. |
| **3.6**<br>**Kutafuta kampuni kwa ajili ya ziara ya kimafunzo: Kwanini huko?** | Vijana wachague kampuni kwa ajili ya ziara ya mafunzo kwa kuzingatia vigezo kadhaa. | Katika jozi, washiriki wajadili ni aina gani ya makampuni (mashirika/biashara ndogo) wanataka kutembelea na kwa sababu gani. Wajadiliane wao kwa wao kile ambacho tayari wanakijua kuhusiana na kampuni hii, wanachotaka kujifunza, jinsi gani inaendana na vipaji vyao na motisha. Waorodheshe mada na maswali wanayohitaji kuuliza, kuyaona au kufanya wakati wa ziara. |

| | | |
|---|---|---|
| **3.7 Ni kampuni gani ninayohitaji kutembelea?** | Vijana wachunguze kampuni wanayotaka kutembelea na kuelezea matarajio yao. | Vijana watakapojua kampuni ambayo wanataka kutembelea, watapata kazi ya kutafuta kwenye mtandao taarifa nyingi kadri iwezekanavyo kuhusu kampuni/sekta/tawi haraka iwezekanavyo. Wahitimishe uchunguzi wao kwa maswali mahsusi wanayotaka kuuliza au mambo fulani ambayo wanataka kuyaona. |
| **3.8 Tafuta kwenye intaneti!** | Vijana wajifunze kupata/ kutafuta taarifa kuhusu makampuni kwenye mtandao. | Pakiwa na simu za kutosha, kompyuta mpakato au kompyuta zilizo na uwezo mzuri wa kutumia mtandao, vijana wafanye mchezo kupata majibu juu ya maswali kuhusu kampuni haraka iwezekanavyo. Maswali kama: wafanyakazi wangapi, jina la mkurugenzi, anwani, namba ya simu, wateja wa kampuni n.k. |
| **3.9 Barua yangu kwa familia yangu** | Vijana waandae ziara yao na kuzijulisha familia zao au marafiki kuhusu ziara hiyo. | Waandike barua kwa wazazi, familia au marafiki zao kuwajulisha kuhusu nini na kwanini wamechagua ziara ya kwenye kampuni. Hii ni fursa kwa vijana kuzungumza na watu kutoka katika mtandao wao binafsi kuhusu kuendeleza fani zao. |
| **3.10 Jiandae!** | Vijana wafanye maandalizi ya utendaji muhimu kwa ajili ya ziara kwenye kampuni. | Kazi binafsi ya kujua namna ya kufika kwenye kampuni, kufika kwa wakati, anwani, namba ya simu, uvaaji n.k. Washiriki washirikishane majibu yao katika kundi. |
| **3.11 Kuangalia nyuma** | Vijana watafakari kama matarajio yao kwenye ziara yao ya kampuni yamefikiwa. | Matarajio yaliyowekwa katika sanduku la 'tazama mbele' yatatolewa moja baada ya jingine. Kila mshiriki atatoa maoni yake juu ya ziara: ulipata, uliona, kusikia nini kilichotarajiwa? Kipi sahihi na kipi sio sahihi? |
| **3.12 Mzunguko** | Vijana watathmini ziara, matembezi yao kwenye makampuni waliyotembelea. | Washiriki wa duara la nje na ndani wahojiane kuhusu yale waliofikiria kuhusiana na safari yao ya kimafunzo. Kila mmoja na masaili na msailiwa. Mizunguko mitano ya mahojiano/ mijadala imefanyika. Baada ya mzunguko, washiriki kutoka duara la ndani watasogea mbele nafasi moja. |
| **3.13 Nimesimama wapi?** | Vijana wapeane uzoefu wao kutokana na ziara ya kwenye kampuni na kutoa tathmini zao. | Vijana wanaweza kuchagua kama wanakubalina au hawakubaliani na kauli tofauti kuhusu ziara yao. Baada ya maelezo, baadhi ya vijana wanaweza kueleza zaidi kwanini wamechagua upande wa kukubaliana au kutokubaliana. |
| **3.14 Mapitio ya ziara** | Vijana watafakari ziara yao: Je, imekidhi matarajio yao? | Vijana waandae wasilisho la dakika 1 -linaloitwa Pitio-ambalo hutoa marejeo juu ya matarajio yao na uzoefu walioupata kwenye ziara yao. Baada ya uwasilishaji wa Pitio wajibu maswali matatu kutoka kwa wanakundi wenzao. |
| **3.15 Taswira ya siku ya kazi** | Vijana watafakari juu ya ziara yao kibunifu. | Vijana watengeneze kipande cha katuni cha siku nzima ya kazi cha mfanyakazi wa kampuni waliyotembelea. Kwa kila aina ya zana, waone wastani wa siku ya kazi. |
| **3.16 Tathmini na shukrani** | Vijana watathmini ziara yao ya mafunzo kwenye kampuni kwa kutuma barua ya tafakuri na shukrani kwa msimamizi/ mkufunzi wa kampuni hiyo. | Kila mshiriki aandae tathmini ya kimaandishi ambayo inaelezea mafanikio, changamoto na mafunzo ya ziara yao kwenye kampuni. Kwa pamoja waandike barua ya shukurani. |

| | | |
|---|---|---|
| **3.17 Daima unajifunza jambo** | Vijana watafakari juu ya vipengele vya fani wanayoipenda zaidi na wasiyoipenda. | Washiriki wote waandae orodha mbili, moja ya masuala ya taaluma/fani wanayopenda zaidi na nyingine ya masuala wasiyopenda sana. Katika jozi watafakari juu ya orodha zao na kujadili inaashiria nini kwa mipango yao baada ya kazi. Wote watoe himisho binafsi. |
| **3.18 Kutafuta kampuni kwa ajili ya mafunzo ya viwandani** | Vijana waanze kwa kuangalia kampuni ambayo wanaweza kufanya mafunzo yao ya viwandani, kwa kuzingatia mahitaji ya programu ya mafunzo ya ufundi, mitihani na mahitaji yao wenyewe. | Vijana wafafanue mahitaji ya mafunzo ya viwandani na nini na kwa vipi wanataka kujifunza. Watafute makampuni matatu ambapo wanataka kufanya mafunzo yao ya viwandani, pia wazingatie vigezo vya shule. |
| **3.19 Mahojiano yangu ya kwanza na kampuni ya mafunzo ya viwandani** | Vijana wajiandae kuwasiliana na kampuni waliyoichagua kwa ajili mafunzo ya viwandani. | Kwa msaada wa maswali kadhaa vijana wajiande kikamilifu kwa ajili ya mawasiliano yao ya kwanza na kampuni. Wafanye hivyo katika vikundi kushirikishana na wenzao maandalizi yao, baadaye somo jingine au igizo linaweza kufanyika. |
| **3.20 Hisia yangu kwanza kwa mafunzo yangu ya viwandani** | Baada ya wiki moja au mbili, baada ya mafunzo ya viwandani vijana watafakari juu ya uzoefu wao wa kwanza. | Kwa msaada wa maswali kila kijana atafakari. Kisha watoe alama kwa kauli nne juu ya mafunzo yao ya viwandani na kushirikishana tathmini hiyo na wanakundi wengine wawili. Wapeane utaratibu kwa ajili ya wiki inayofuata watakaporudi kwenye mafunzo ya viwandani. |
| **3.21 Nina ustadi wa kutosha?** | Vijana wabadilishane changamoto ambazo wanaweza kukutana nazo kazini na kujadili njia tofauti za kukabiliana nazo. | Baadhi ya changamoto zimetolewa na wakati wa mjadala sehemu zote za changamoto zisisitizwe. Vijana watazame sintofahamu hizo kwa mtazamo tofauti na watagundua kuwa kuna njia mdabala za kukabiliana nazo. Vijana wanaweza pia kutambulisha changamoto zao wenyewe. |
| **3.22 Barua yangu kuhusu uzoefu wangu wakati wa mafunzo ndani ya kampuni** | Vijana watafakari juu ya uzoefu wao wa mafunzo ndani ya kampuni katika wiki zilizopita. | Vijana waandike barua kwa mtu wanayemjua na kumwambia kuhusu uzoefu wao na mafunzo yao. Mada ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi zitolewe. Waombe jibu au mazungumzo mafupi juu ya maudhui ya barua. |
| **3.23 Picha zinazowakilisha mafunzo yangu ndani ya kampuni** | Vijana waoneshe siku ya kazi inaonekaje na ni kipi wanakipenda sana au kukipenda kidogo. | Vijana watengeneze vipeperushi kwa kila aina ya vifaa/zana (kwenye karatasi au kidijitali) kuhusu uzoefu wao wakati wa mafunzo ya viwandani. Wawasilishe vipeperushi hivyo kwenye kundi na kutolea maelezo. |
| **3.24 STARR-mbinu ya kutoa maana ya uzoefu** | Vijana watafakari juu ya tukio ambalo lilikuwa muhimu kwao wakati wa mafunzo yao ya viwandani na ambalo walitumia vipaji na ujuzi wao. Wanajifunza kutoa maana ya uzoefu huo. | Kwa kutumia mbinu ya STARR vijana watafakari juu ya tukio fulani. Wachambue yafuatayo: Hali, Jukumu, Shughuli, Matokeo na Tafakuri. Katika kundi la watu watatu, kila mshiriki apate wasaa wa kuhoji, kutaarifu na kutafakari juu ya moja wapo ya uzoefu wao. |

3.1

# JE, FAMILIA YANGU INA AINA GANI YA KAZI?

KARATASI YA ZOEZI 3.1

**Lengo**
Vijana wagundue aina ya kazi za wanafamilia yao na kutambua ushawishi wa kazi za kawaida/biashara katika familia zao juu ya vipaji vyao, shauku na malengo ya kazi zao wenyewe.

**Maandalizi**
Tengeneza mchoro wa ukoo wako mwenyewe na shughuli zote/kazi/biashara ya baba yako, mama na wanafamilia wengine ambao ni muhimu kwako. Unaweza kufikiria kuanzia kwa mababu zako kutoka pande zote mbili, wajomba zako na shangazi wanachofanya au kutafakari nini kaka zako na dada zako wanachotaka kufanya ukubwani. Unaweza kutumia karatasi ya zoezi 3.1 'Mti wa familia' au kuchora mchoro wa ukoo wako na karibu na pembeni yake ukaweka mchoro wa mti wa kisiwa chako au eneo ambalo unaishi. Hakikisha kuna karatasi za kutosha za zoezi 3.1 (aina ya A2) na zana za kuchorea.

**Maelezo**
'Baadhi ya watu katika umri mdogo kabisa tayari wanajua wanataka kuwa nani ukubwani. Kwa wengine, ni ngumu sana kupata fani na elimu inayowafaa zaidi. Je, unajua nini familia yako inafanya kwa ajili ya kuendesha maisha? Je, unatambua jinsi mfumo wa maisha wa ndugu zako ulivyoathiri maamuzi yako mwenyewe? Kupitia zoezi hili unaweza kuyabaini yote hayo. Unaweza ukafanya uvumbuzi fulani wa kuvutia!'

**Utendaji**
1. Waelekeze vijana watengeneze mchoro wa mti wa familia, tumia mfano kwenye karatasi ya zoezi 3.1 'Mti wa Familia' kuwawezesha kutumia mchoro wenyewe. Familia inaweza kufanywa kubwa kadri vijana wanavyotaka iwe, yenye wazazi wengi na (nusu) kaka na dada; angalia wanafamilia wote wa kike kwa wa kiume. Waache waandike jina na taaluma au biashara ndogo ya kila mwanafamilia. Pia tazama njia zisizo rasmi za kupata pesa.
2. Ikiwa mti wa familia umekamilika, waombe vijana kuwashirikisha wenzao mchoro wa ukoo. Waulize kutafakari juu ya ukoo wao kwa kushirikishana majibu juu ya maswali kama:
   - Ni nini kinapungua unapoangalia kazi/shughuli za wanafamilia wako?
   - Je, kuna mwenendo fulani unaoonekana? Je, kuna mambo fulani ambayo yanafanana? Kuna tofauti gani?
   - Ni kitu gani unakipenda katika mambo mbalimbali ili wewe uweze kuishi vizuri au kazi mbalimbali unazoweza kuwa nazo? Ni kitu gani hukipendi?
   - Ni mabadiliko gani unataka kuyafanya wewe mwenyewe? Kwanini?
3. Acha kila mmoja aandike kwa kifupi kile ambacho amegundua kulingana na michoro ya koo zao. Waache wafanye baadhi ya hitimisho kuhusiana na kazi zao wenyewe.

**Tafakuri**
Katika kikundi, mnaweza kujadili uvumbuzi na hitimisho kama matokeo ya kutengeneza mchoro wa ukoo na kwa kushirikishana matokeo katika jozi. Waulize vijana kile wanachotaka kufanya. Je, watafuata nyayo za wazazi au babu zao? Maoni yao ni nini? Je, watafanya nini sawa na/au watafanya nini tofauti? Je, bado inawezekana kuwa na kazi sawa kama ilivyofanyika katika familia zao? Ni mabadiliko gani wanayoyaona katika soko la ajira na katika jamii kwa ujumla? Je, hiyo ina maana gani kwa kazi zinazopatikana au kwa kuanzisha biashara zao wenyewe?

***Dondoo***
Kama vijana hawawezi kukamilisha mchoro wa ukoo wao, kwa sababu hawajui majina au fani zao, wanaweza kwenda na michoro yao nyumbani na kuuliza familia zao ili kupata msaada. Hii ni njia nzuri ya kuhusisha familia zao katika mchakato wao wa kufanya maamuzi na uendelezaji wa fani zao.

# 3.2 MAHOJIANO NA MWANAFAMILIA

## Lengo
Vijana wachunguze njia ambazo ndugu zao wamezitumia kupata kazi mpaka sasa. Wajifunze pia ni muhimu na inavutia kiasi gani kuwa na mazungumzo na mtu mwingine kuhusu fursa za ajira na kazi.

## Maandalizi
Jiandae kwa kufikiria kuhusu maswali mazuri ambayo unaweza kuwauliza watu kuhusu kazi zao. Unafikiria nini kuhusu maswali yaliyotolewa katika dondoo? Je, unakosa baadhi ya maswali? Je, kuna maswali katika orodha ambayo labda sio heshima kuuliza? Boresha orodha na fikiri juu ya mtiririko mzuri zaidi. Mnapojadili matokeo ya mahojiano, ni vyema kuwa na projekta kwa ajili ya vijana wanaotaka kuonesha picha za video/picha ya mahojiano yaliyorekodiwa.

## Maelezo
'Watu wengi hupenda kuzungumza juu ya taaluma zao na kazi zao. Familia yako pia ni sehemu ya mtandao wako; unaweza kujifunza mengi kutoka kwao na inakufumbua juu ya unachopenda kuhusu kazi zao na unachotaka kufanya tofauti. Unajua familia yako inajishughulisha na nini kuendesha maisha? Kwa kumhoji mmoja wao, utajifunza kutoka kwao. Katika somo hili, utaandaa mahojiano, baada ya hapo utahojiana na mwanafamilia wako na kuwasilisha matokeo darasani. Labda unaweza kugundua kitu kizuri!'

## Utendaji
1. Waandae vijana kwa mahojiano na mmoja wa wanafamilia wao. Wafafanulie kwamba maandalizi mazuri kabla ya mahojiano halisi ni muhimu ili kupokea majibu yatakayofaa. Maandalizi mazuri ni nusu ya pambano, hata kama wanajuana na mwanafamilia.
2. Acha vijana wachague mwanafamilia wanayetaka kumhoji juu ya kazi zao. Ni kwanini alifanya kazi hiyo au jinsi gani alivyopata kazi hiyo.
3. Kwanza lipe kundi lako kazi ya kuandaa orodha ya maswali ya kuuliza kwenye mahojiano.
4. Waruhusu washirikishane maswali yao katika kundi la watu wanne na uwaombe kuandaa orodha moja ya mwisho.
5. Badilisha maswali ya vikundi vingine katika kundi zima: kundi lisome swali moja kwa sauti, liandike kwenye chati mgeuzo (ubaoni) na kisha kundi jingine litoe swali jingine mpaka maswali yote yaandikwe. Ruka maswali yote yanayofanana.
6. Tafakari juu ya mtiririko wa maswali kwa ajili ya mahojiano mazuri. Nini kianze kuulizwa, nini kifuate na nini kiwe cha mwisho? Kwanini?
7. Ruhusu kila mmoja aandae karatasi yake ya mahojiano na maswali yatakayomfaa mwanafamilia kuyajibu na mistari myeupe kwa ajili ya majibu.
8. Jiridhishe ni lini mahojiano yatafanyika. Toa maelekezo sahihi ni ripoti gani unayotaka kuhusu mahojiano. Toa tarehe na wakati gani matokeo yatajadiliwa darasani.

## Tafakuri
Matokeo ya mahojiano yanaweza kufanyika kwenye makundi ya watu wawili wawili au wanne wanne. Washiriki wanaweza kuambizana waliyojifunza. Maswali tarajali wanayoweza kujibu ni: Wanapendelea kujadili aina yao ya kazi na mtu kutoka katika familia zao? Je, wamewahi kufanya hivyo kabla? Je, wamegundua mambo ambayo hawakujua kabla? Je, walipata majibu au mapendekezo ambayo ni ya manufaa zaidi? Je, kuna mambo ya kustaajabisha waliyokutana nayo wakati wa mahojiano? Baada ya kushirikisha katika vikundi, matokeo yanaweza kujadiliwa au kuoneshwa (picha au sehemu za video) katika kundi zima.

### *Dondoo*
Washiriki wanahitaji kufanya orodha yao ya maswali ya mahojiano na wanafamilia wao. Mapendekezo ni:
- Unafanya nini katika kazi yako?
- Unapenda nini kuhusu kazi yako?
- Nini hukipendi kuhusu kazi yako?
- Ni sifa gani unapaswa kuwanazo ili kufanya kazi hii vizuri?
- Je, mnafanya kazi kwa kushirikiana sana? Je, ungependa kufanya kazi katika timu?
- Tangu lini ulibaini unataka kufanya kazi hii?
- Ulijuaje kama unataka kufanya kazi hii?
- Ulijiandaje kwa kazi hii? Ulifanyaje kuelewa ?
- Ulikuwa na elimu gani?
- Je, elimu hiyo ina mchango katika kazi unayofanya sasa?
- Ni kazi gani nyingine ulizofanya hadi sasa?
- Ulipenda nini kuhusu hilo?
- Je, una vidokezo vyovyote vinavyoweza kutengeneza na kukuza kazi yangu?

Ikiwa vijana wamependa wazo hili: Waache wapige picha na mwanafamilia wakati au baada ya mahojiano. Au toa kazi kwamba vijana wajirekodi filamu kwa simu wakati wanapozungumzia mambo mawili waliyopenda zaidi kuhusu kufanya mahojiano haya na kuhusu kile walichojifunza kutokana na mahojiano haya. Kipande hiki cha filamu kitatumika wakati wa kujadili zoezi baadaye.

## Uchunguzi wa kina
Ikiwa vijana pia walifanya zoezi la 4.3 'Je mtandao wangu (wa kweli) unaonekana katika sura ya 4 'Gundua mtandao yako', wanaweza pia kufanya zoezi hili na mtu 1 kati ya 2 kutoka kwenye mtandao wao (wa kweli). Hayo labda hufanya mahojiano yawe rahisi sana kufanyika, lakini kwa sababu hii washiriki wanaweza kuona nini cha kufanya kwa kutumia mtandao wao kwa ajili ya maendeleo yao ya kazi. Inawezekana pia wataona kuwa watu wengine mara nyingi sana wako tayari kushirikiana katika mahojiano au kazi hizo.

# 3.3

# MASWALI YANGU KWA MTAALAMU

KARATASI YA ZOEZI 3.3

**Lengo**
Vijana waandae mahojiano na mtaalamu. Katika somo moja au zaidi, watafanya mahojiano haya na mtu kutoka tawi au sekta inayowavutia zaidi.

**Maandalizi**
Kwa zoezi hili, itafaa zaidi ikiwa wewe au taasisi yako mtawajua wataalamu kadhaa katika maeneo mbalimbali ambao wako tayari kuhojiwa. Ikiwa sio hivyo, vijana waangalie katika mtandao wao ili kupata wataalamu ambao wako tayari kuhojiwa wakati wa kipindi. Fikiria kuhusu wataalamu wangapi ambao wanaweza kuhojiwa wakati wa somo moja. Fanya makubaliano nao kuhusu tarehe watakazopatikana kwa mahojiano. Chapisha karatasi ya zoezi 3.3 'Maandalizi ya kumhoji mtaalamu'.

**Maelezo**
'Wataalam ni watu bora kukuambia nini maana ya kufanya kazi zao kila siku. Wanajua vizuri zaidi kile unachokitarajia unapopata kazi katika kampuni au wakati unapotaka kuanzisha biashara mwenyewe. Ili kuhakikisha kuwa unapata kadri iwezekanavyo kuhusu kile kinachokuvutia, tutaandaa orodha ya maswali ambayo unaweza kumuuliza mtaalamu. Kwa njia hii, una uhakika wa kupata maelezo unayotaka na unayohitaji.'

**Utendaji**
1 Lipe kundi lako orodha ya wataalamu ambao wako tayari kuhojiwa. Waulize washiriki wako kuongeza kwenye orodha ya wataalamu wanaowajua kutoka kwenye mitandao yao wenyewe.
2 Waelekeze washiriki watengeneze orodha binafsi ya maswali 6 ambayo wanataka kumuuliza mtaalamu aliechaguliwa.
3 Toa nadharia na dondoo kuhusu maswali ya wazi na maswali yaliofungwa.
4 Andaa makundi ya washiriki watatu ambao wana aina moja ya mtaalamu katika fikra. Acha waijadili orodha yao na kwa pamoja watengeneze orodha moja kwa kila kundi yenye angalau maswali 10.
5 Waache waandae rasimu ya orodha hii na warekebishe maswali na mtiririko wake mpaka waridhike. Baada ya hapo waandike orodha hiyo kwenye karatasi ya zoezi 3.3 'Maandalizi ya kumhoji mtaalamu'.
6 Andaa sheria inayoeleweka juu ya wakati gani wataalamu wanapaswa kuhojiwa (wiki na vipindi gani) na wape vijana hizi tarehe.
7 Wakati wataalamu wamefika tayari kuhojiwa, vikundi vya watu watatu ambao walitengeneza orodha maalumu ya maswali katika kada hiyo, wafanye mahojiano mbele ya darasa.
8 Waache washiriki wengine washiriki kipindi cha mahojiano. Fikiri nao kwa pamoja juu ya hoja zinazojitokeza na waandike wanachokiona.

**Tafakuri**
Waulize vijana walivyopendezewa kutengeneza orodha hii ya maswali kwa mtaalamu. Kipi kilikuwa rahisi, na kipi kilikuwa kigumu kwao? Je, kulikuwa na maswali ambayo hayakuwekwa kwenye orodha? Ikiwa ndivyo, imekuaje? Mara baada ya mahojiano unaweza kuuliza makundi ya washiriki watatu waliyofikiria kufanya mahojiano. Je, hali ilikuwaje wakati wa mahojiano? Ni taarifa gani waliyokusanya? Je, kuna mambo ambayo yaliwashangaza? Je, kuna mambo ambayo yaliwaduwaza? Zaidi ya hayo, waombe watafakari juu ya ujuzi wao wa mahojiano na nini walipenda kuhusu hayo? Muulize mtaalamu kile alichopenda juu ya mahojiano na muombe vidokezo ili kuboresha. Waambie watazamaji watoe maoni zaidi juu ya maudhui ya mahojiano na kutoa mrejesho juu ya kile walichodhani wasaili walifanya vizuri na wanachoweza kufanya vizuri zaidi.

***Dondoo***

Wahimize vijana kuja na maswali ambayo sio ya kutoa jibu la 'ndiyo' au 'hapana' wakati wote; katika hali hiyo daima wanahitaji kuuliza maswali mapya. Wapatie mifano kadhaa ya maswali ya wazi, ambayo huanza, na 'nini', 'vipi' au 'kwanini'. Au 'Je, unaweza kuniambia zaidi kuhusu ....?' Andaa mahojiano kwa kutoa vidokezo vya kimawasiliano: mfano jinsi ya kukaribisha mtaalamu, jinsi ya kufanya utambulisho, jinsi ya kufanya maswali kuwa wazi, jinsi ya kufupisha na jinsi ya kumshukuru mtaalamu kwa muda wao mwishoni? Fanya maandalizi haya kuhusu sheria za mawasiliano muda mfupi kabla ya mahojiano kufanyika. Sisitiza kwamba vijana wanaweza kuuliza swali lolote ambalo wanataka, lakini mtaalamu anaweza kusema yeye hataki kujibu swali hilo. Aidha, mahojiano si lazima yawe rasmi sana. Lengo la vijana ni kukusanya taarifa nyingi za kuvutia kadri iwezekanavyo kuhusu kazi au biashara.

**Uchunguzi wa kina**
Itakuwa vizuri kurudia zoezi mara kadhaa. Kisha vijana watakuwa na ujuzi zaidi wanapokuja kuchagua kazi zao pendwa. Pia, wakati masomo yao yanaendelea, labda watahitaji kupata habari zaidi au tofauti. Mara ya pili wanaweza kufanya maandalizi ya kila mmoja au kwa makundi ya watu watatu, wanaweza kumualika mtaalamu kutoka kwenye mtandao wao binafsi (wataalamu wanaowafahamu), kuweka miadi, kwenda kumtembelea mtu na kufanya mahojiano. Hata hivyo, daima fanya tathmini ya baadaye katika kikundi. Mazungumzo na watu kutoka mazingira ya kazi pia yanaweza kufanyika wakati wa ziara ya kampuni na/au wakati wa mafunzo ya viwandani. Mapendekezo ya maswali katika mada:

- Kampuni yenyewe;
- Kazi na shughuli ambazo mtaalamu lazima afanye;
- Mafunzo ya elimu ya lazima na fursa za mafunzo ya ziada katika kampuni;
- Wafanyakazi wengine wa kampuni/wenzako wa moja kwa moja;
- Haki na majukumu ya mtaalamu, dondoo na mbinu kutoka kwa mtaalamu.

3.4

# KUTARAJIA ZIARA YA KIMAFUNZO

**Lengo**
Vijana wachunguze matarajio yao kuhusu ziara: kutembelea kampuni, shirika au biashara ndogo.

**Maandalizi**
Kwa zoezi hili, unahitaji sanduku la kasha au bakuli zuri lenye neno, 'tazama mbele' liwe limechapishwa au kubandikwa juu. Zaidi ya hayo, wakufunzi wanahitaji kujua ni makampuni/ mashirika au biashara ndogo vijana wanaweza kutembelea inapowezekana. Pia ni vizuri kama unaweza kutaja kama mfano baadhi ya matarajio ya vijana: 'Nataka kuangalia vipaombele vya kampuni, Nataka kujua siku ya kazi nyingi inakuaje, Nataka kuona kampuni nzima na kuitembelea mazingira yake, Ninataka kujua wenzangu ninaotakiwa kufanya nao kazi pamoja' na 'Nataka kujua wateja wa kampuni hii ni akina nani'.

**Maelezo**
'Ni muhimu kujua matarajio uliyonayo kabla ya kutembelea kampuni ili kupata iwezekanavyo mafanikio ya ziara yako. Kwanini? Unapojua unachotaka, ndivyo maswali yako yatakavyozidi kuwa bora na utajua zaidi nini cha kuangalia wakati ukiwa unatembea kwenye kampuni. Ikiwa unafikiri: 'Nitaenda tu na kuona chochote kinachotokea', unaweza kurejea nyumbani na hisia kuwa hukufanikiwa kwa chochote. Katika zoezi hili, utatengeneza matarajio yako juu ya ziara zako za wazi.'

**Utendaji**
1. Chukua sanduku, kopo, au bakuli na waambie vijana kwamba unahitaji kukusanya matarajio yao kuhusiana na ziara na kuyaweka kwenye kasha.
2. Pata mifano ya matarajio ambayo wanafunzi wanaweza kuwa nayo, kama ilivyopendekezwa hapo juu katika 'Maandalizi'. Unaweza kutoa mifano, wakati vijana wanapokuwa wagumu kutekeleza, lakini ni bora zaidi wakati wanapojitokeza wenyewe.
3. Mpe kila mwanafunzi vipande vitatu vya karatasi na waelekeze kila mmoja kuandika jina lake na tarajio moja juu ya ziara hiyo.
4. Waelekeze kushirikishana matarajio yao katika jozi.
5. Waruhusu vijana wasome matarajio yao mbele ya darasa na baadaye wakaweke vipande vyao vya karatasi kwenye kasha.
6. Wajulishe kwamba utafungua kasha baada ya ziara na kuona matarajio ambayo yameonekana kuwa sahihi. Weka tarehe ya mwisho ya tukio hili.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanavyojisikia kuhusu jinsi walivyoandaa ziara yao katika kampuni. Nini kitakuwa athari ya maandalizi haya? Ilikuwaje kusikia kuhusu matarajio ya washiriki wenzake?

***Dondoo***
Baada ya ziara ya kampuni, fanya zoezi la 3.11 'Kuangalia nyuma'.

# KAMA IWAVYO KAZINI!



**Lengo**
Vijana wagundue ujuzi waliopata katika kazi zao zisizo rasmi na kuchunguza matarajio yao kuhusu ziara ya kutembelea kampuni.

**Maandalizi**
Weka meza darasani katika sura ya U ili vijana waweze kutazamana. Hakikisha kuna karatasi ya kufanyia kazi, karatasi kubwa na kalamu za wino mzito. Hakikisha una karatasi za kutosha za zoezi 3.5 'Uzoefu wangu wa kazi mpaka sasa'.

**Maelezo**
'Katika maisha yetu ya kila siku, tumejifunza ujuzi mwingi kwa kufanya kazi nyumbani, shambani au kwenye biashara za wazazi au marafiki. Kwa zoezi hii, tutaangalia ujuzi huo na kile tulichojifunza. Baada ya hapo tutaangalia nini unatarajia kutoka katika ziara ya kutembelea kampuni. Unadhani kuwa ujuzi au maarifa uliyopata unaweza kutumika katika mazingira rasmi zaidi? Kutakuwa na tofauti au mfanano upi katika kazi unazofanya katika mazingira mawili tofauti? Matembezi katika kampuni yanalenga kupata wazo sahihi kuhusu kazi na mahitaji. Aidha inakuwezesha kuuliza maswali kwa watu mbalimbali na hivyo kupata taarifa unayoihitaji.'

**Utendaji**
1. Waulize vijana walio na uzoefu wa kazi katika sekta isiyo rasmi: katika kaya, shambani, kwenye kampuni ya wazazi/marafiki zao au kazi za muda/likizo. Andika aina tofauti za uzoefu wa kazi kwenye karatasi kubwa/ubao.
2. Ligawe kundi katika makundi ya watu watatu watatu na waache washirikishane majibu yao kwa maswali kwenye karatasi ya zoezi 3.5 'Uzoefu wangu wa kazi mpaka sasa':
   - Ni ujuzi au ustadi gani ulioupata wakati wa kazi yako ya zamani?
   - Ni tofauti gani na mfanano gani unaona kati ya uzoefu wako wa kazi zako binafsi na kazi rasmi?
   - Unafikiri kampuni itatarajia nini kutoka kwako unapoanza kazi yako rasmi pale?
3. Katika darasa vijana wajadili majibu yao na waandike maneno muhimu kwenye karatasi kubwa.
4. Baada ya mjadala wa darasani, waulize vijana kile wanachotarajia kutokana na ziara yao. Waache waandike hii kwenye karatasi ya zoezi 3.5 au tumia 'Sanduku la kutazama mbele' katika zoezi 3.4.

**Tafakuri**
Waulize washiriki jinsi wanavyojisikia kutafakari juu ya uzoefu wao wa kazi za awali. Je, vipi kuhusu maandalizi ya ziara (ya kimasomo)? Je, vijana watafanya nini ili kuhakikisha matarajio yao yanatimizwa? Weka tarehe ya kutathmini ziara ya kampuni.

Baada ya kutembelea kampuni utaitathmini. Tafakuri hii inaweza kuunganishwa na zoezi 3.11 'Kuangalia nyuma' ambapo sanduku au kasha lenye matarajio linaweza kufunguliwa tena. Je, matarajio yalitimizwa? Kama ndiyo, walipata uzoefu gani? Ikiwa sio, ilisababishwa na nini? Je, waliona kitu chochote maalum? Je, palikuwa na matukio ya kushangaza au kuwagusa wao? Je, kulikuwa na vitu ambavyo walitaka kujua au kuvizungumzia zaidi?

***Dondoo***

Tumia muda wa kutosha kuzungumza juu ya kile walichojifunza vijana hadi sasa kutokana na uzoefu wao wa kazi mbalimbali, za kulipwa au kutolipwa. Sisitiza kwamba ujuzi na uwezo ambao wamepata tayari huongeza kujiamini na uelewa wao binafsi. Stadi binafsi unazozipuuza zinaweza kuonekana kuwa za thamani zaidi na ya pekee kuliko uliyofikiri awali. Jaribu kuwaelewesha vijana ukweli kwamba kutembelea katika kampuni kutafanikiwa iwapo watakuwa wadadisi zaidi wakati wa matembezi yao. Je, matarajio yao ni yapi? Wana maswali gani? Unaweza kuchanganya zoezi hili na zoezi 3.4 'Kutarajia ziara ya kimafunzo'.

3.6

# KUTAFUTA KAMPUNI KWA AJILI YA ZIARA YA KIMAFUNZO: KWANINI HUKO?

**Lengo**
Vijana wachague kampuni kwa ajili ya ziara ya mafunzo kwa kuzingatia vigezo kadhaa.

**Maandalizi**
Kwa zoezi hili, itafaa sana ikiwa wewe na taasisi yako mnajua kampuni/mashirika/biashara ndogo ndogo zitafaa kwa ziara na kitu gani wanaweza kutoa. Hakikisha una orodha ya makampuni ambayo umefanya kazi kabla. Bila shaka, vijana wanaweza pia kuangalia mtandao wao wenyewe ili kupata kampuni inayofaa. Panga meza na viti ili vijana waweze kufanya kazi kiurahisi kwa makundi ya watu wawili au watatu. Hakikisha una karatasi kubwa au ubao. Toa nakala nyingi za karatasi ya zoezi 3.6 'Matarajio yangu kuhusu ziara ya kampuni' kulingana na mahitaji yako.

**Maelezo**
'Lengo la kutembelea kampuni ni kupata maoni juu ya kazi zinazotarajiwa baadae na kuongeza uelewa namna ilivyo siku ya kawaida ya kazi. Ni muhimu zaidi ikiwa unatembelea kampuni ambayo unaipenda. Kwa hiyo, una nafasi kubwa zaidi ya kupata habari za thamani. Katika zoezi hili, tutachunguza makampuni ambayo ungependa kutembelea na sababu zake.'

**Utendaji**
1. Ligawe kundi katika makundi ya watu wawili au watatu.
2. Wapatie vijana orodha ya makampuni wanayoweza kuchagua na wayajadili makampuni ambayo yanawavutia na kwanini. Pia wanaweza kutembelea makampuni kutoka kwenye mtandao wao wenyewe (wazazi, jamaa, majirani). Ikibidi, vijana wanaweza kutafuta kwenye intaneti (mtandao) makampuni yanayowavutia kutembelea.
3. Acha vijana wachague kampuni moja ambayo wangependa kutembelea kutoka kwenye makampuni yaliyopo.
4. Andika maswali ubaoni (au andaa karatasi ya zoezi) na waruhusu vijana kujadili kwanini wamechagua kampuni ipi, wakitumia maswali yafuatayo:
   - Ninataka kujifunza zaidi katika taaluma au kazi gani?
   - Ni kwa namna gani ninaweza kutumia vipaji vyangu katika kazi hii?
   - Ninapenda nini kuhusu fani au kazi hii?
   - Sipendi nini kuhusu fani au kazi hii?
   - Nina mashaka gani?
   - Tayari ninajua nini kuhusu kampuni hii?
   - Nataka kujua nini zaidi kuhusu kampuni hii?
5. Mwishoni mwa majadiliano kila mwanafunzi anapaswa kujaza karatasi ya zoezi 3.6 'Matarajio yangu kuhusu kutembelea kampuni'.
6. Weka tarehe mbili, moja kwa ajili ya ziara kwenye kampuni na nyingine mtatathmini matembezi na vijana kwenye kampuni. Andika tarehe mbili kwenye karatasi kubwa/ ubaoni. Toa maelekezo sahihi ni ripoti gani unayotaka kuhusu mahojiano.

**Tafakuri**
Ilikuwaje kwa vijana kujiandaa kutembelea kampuni kwa namna hii? Je, waligundua mambo mapya wakati wa maandalizi?Baada ya kutembelea kampuni kuna tathmini. Tathmini hii inaweza kuunganishwa na zoezi 3.11 'Kuangalia nyuma' wakati sanduku, kasha, au bakuli lenye matarajio litakuja kufunguliwa tena. Je, matarajio yao yametimilika? Je, maswali yamejibiwa? Je, walijifunza mambo ambayo hawakujua kabla? Yapi na kwa jinsi gani?

Upimaji wa zaida na tafakuri unaweza kuzikuwa kwenye majumuisho.

***Dondoo***
Sisitiza kuwa ni muhimu kwa vijana kufikiri mbali na wanayotarajia watakapotembelea kampuni. Kwa kufanya hivyo vijana wanaweza kuuliza maswali sahihi wakati wa ziara yao na kukusanya taarifa ambayo ni muhimu kwao. Pia matarajio yanaweza kuhifadhiwa katika sanduku la matarajio katika zoezi 3.4 'Kutarajia ziara ya kimafunzo'.

3.7

# NI KAMPUNI GANI NINAYOHITAJI KUTEMBELEA?

**Lengo**
Vijana wachunguze kampuni wanayotaka kutembelea na kuelezea matarajio yao.

**Maandalizi**
Kwanza, unahitaji kujua ni makampuni gani yanaweza kutembelewa. Je, wewe au taasisi yako ina orodha ya makampuni ambayo wanataka kutoa fursa ya kufanya ziara? Kisha fanya zoezi mwenyewe, kuhakikisha kuwa taarifa zote unazotaka washiriki kupata zinapatikana kwenye tovuti ya kampuni watakayotembelea. Andika maswali kwenye ubao kabla, na vijana wanaweza kutoa maswali na majibu katika madaftari yao. Andaa karatasi ya zoezi 3.6 'Matarajio yangu kuhusu ziara ya kampuni', nakala nyingi kulingana na uhitaji.

**Maelezo**
'Maandalizi mazuri ni nusu ya mapambano! Ukiwa umejiandaa vizuri kwa ajili ya ziara ya kampuni, utakuwa na uhakika wa kupata taarifa unazotaka. Bila maandalizi mazuri, inamaanisha kwamba unaona kinachotokea na kwamba unaruhusu wengine kuamua unayofanya, unakuwa katika hatari ya kuwa na ziara ya kampuni ambayo haifai. Bila shaka, unataka kuyaepuka, kwa sababu hiyo itakuwa ni kupoteza muda wako na wa kampuni. Baadaye unapoenda kwenye usaili wa kazi ni muhimu kufanya utafiti mzuri kabla.'

**Utendaji**
1 Waelekeze vijana kuangalia tovuti ya kampuni wanayotembelea na waache waandike maswali yafuatayo:
- Kampuni iko wapi?
- Kampuni inafanya nini?
- Kampuni hii ni nzuri, katika lipi?
- Kampuni hii inataka kufanikisha nini?
- Ni watu wangapi wanaofanya kazi katika kampuni hii?
- Mmiliki wa kampuni ni nani?
- Ni kazi gani zinazoweza kupatikana katika kampuni?
- Wateja ambao kampuni hufanya nao kazi?
- Umepata nini cha kushangaza kuhusu tovuti?
- Unapata hisia gani kutoka kwa kampuni?
- Je, una maswali gani baada ya kuona tovuti nzima?
- Unatarajia kuona/kupata uzoefu gani katika kampuni hii?
- Unatarajia nini?
- Nini kinaonekana kukufurahisha?
- Kipi umeona kinatisha?

2 Waelekeze vijana washirikishane majibu waliyoyapata katika jozi au katika kundi moja ambalo wanakwenda kutembelea kampuni.
3 Kama zoezi la hitimisho, vijana wanaweza kujaza karatasi ya zoezi 3.6 'Matarajio yangu kuhusu ziara ya kampuni'.
4 Weka tarehe mbili, moja kwa ajili ya ziara ya kampuni na nyingine mtakayotumia na vijana kutathmini matembezi yenu kwenye kampuni. Andika haya kwenye karatasi kubwa/ubaoni. Toa maelekezo sahihi ni ripoti gani unayoitaka ya nyuma kuhusu mahojiano.

**Tafakuri**
Waulize vijana kama zoezi hili lilikuwa na maandalizi mazuri ya ziara ya kampuni, na kama bado kuna taarifa wanakosa. Wahimize kushirikisha maandalizi yao kwenye familia zao, kuwataarifu kuwa wanaweza pia kupata msaada. Tathmini itafanyika baada ya ziara ya kampuni. Tathmini hii inaweza kuunganishwa na zoezi 3.11 'Kuangalia nyuma' wakati sanduku au kasha la matarajio litapofunguliwa tena. Wameionaje ziara hiyo? Je, kulikuwa na kitu kama walichotarajia? Wamejifunza nini ambacho ni muhimu kwa fani zao wenyewe? Je, walizungumza kuhusu ziara na wazazi, marafiki, ndugu zao? Maoni yao yalikuwa yapi?

Njia nyingine za kutathmini na kutafakari zinaweza kupatikana katika maelezo.

***Dondoo***
Tafuta kama majibu yote yanaweza kupatikana kwenye mtandao (intaneti). Waelekeze vijana waioneshe tovuti katika familia na marafiki na kuwajulisha kuhusu kampuni watakayotembelea. Matarajio yanaweza pia kuhifadhiwa kwenye 'sanduku la matarajio' katika zoezi 3.4 'Kutarajia ziara ya kimafunzo'.

# 3.8 TAFUTA KWENYE INTANETI!

**Lengo**
Vijana wajifunze kupata/kutafuta taarifa kuhusu makampuni kwenye mtandao.

**Maandalizi**
Kwa zoezi hili, ni muhimu kila mtu awe na kompyuta au kompyuta mpakato; inawezekana pia kutumia simu ya mkononi. Endapo hapatakua na kompyuta/laptop za kutosha au simu za mkononi, wanaweza kuendelea kufanya hivyo kwenye vikundi, badala ya mtu mmoja mmoja. Alama lazima zihifadhiwe kwa sababu mshindi wa mchezo huu atatangazwa. Chagua kampuni ambayo ina tovuti nzuri. Unahitaji kujihakikishia kwamba inawezekana kupata kwenye tovuti hii majibu yote kwa maswali yafuatayo. Ikiwa sio, unahitaji kubadilisha swali hili. Andaa orodha ya alama kwenye ubao.

**Maelezo**
'Mchezo wa kujifurahisha 'Tafuta hili' unaweza kufanyika ili kujua zaidi kuhusu kampuni. Lengo la mchezo huu ni kupata majibu kwenye mtandao haraka iwezekanavyo. Maswali yatakuwa kuhusu moja ya kampuni tutakayotembelea. Kila swali litaulizwa moja baada ya jingine. Na yule ajuae jibu la swali hilo, atasema kwa sauti: 'Acha!'.'

**Utendaji**
1. Hakikisha kila mmoja ana kompyuta, simu na kufungua ukurasa wa Google. Pakikosekana kompyuta au simu za kutosha, uwagawanye katika makundi madogo madogo kulingana na idadi ya vifaa vilivyopo.
2. Watake vijana kutafuta majibu ya maswali yafuatayo kuhusu kampuni (tahadhari: Umeangalia ikiwa majibu yote yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya kampuni):
   - Ni wafanyakazi wangapi wako kwenye kampuni?
   - Anwani ya kampuni ni ipi?
   - Mmiliki wa kampuni ni nani?
   - Taja majina ya kazi tano zipatikanazo kwenye kampuni hii.
   - Taja wateja watatu/wateja wa kampuni.
   - Kampuni ilianza mwaka gani?
   - Nambari ya simu ya kampuni ni ipi?
3. Wakati mshiriki au kikundi kidogo kikipata jibu kwa swali husika, waseme kwa sauti 'Acha!'.
4. Endelea kuangalia jibu na kuweka alama kwenye ubao, ili uweze kumpata mshindi.

**Tafakuri**
Waulize vijana jinsi wanavyojisikia kuhusu mchezo. Je, wanajisikiaje kuhusu kuangalia kwenye tovuti ili kugundua ulimwengu wa kazi, kuandaa ziara za mafunzo au kuomba kazi?

***Dondoo***
Hakikisha kwamba majibu ya maswali yako yanaweza kupatikana kwenye mtandao. Toa tuzo ndogo kwa mshiriki ambaye ni mshindi/kundi ambalo mafanikio yatakuwa mazuri. Unapojua kuwa washiriki wengi hawana uelewa na Google au mtandao, hakikisha kwanza unapanga kipindi cha kujifunza kuhusu Google na mtandao/intaneti. Waache wafundishane kuhusu mtandao na jinsi ya kupata taarifa kwenye wavuti. Baada ya hapo, unaweza kuanza zoezi hilo.

3.9

# BARUA YANGU KWA FAMILIA YANGU

**Lengo**
Vijana waandae ziara yao na kuzijulisha familia zao au marafiki kuhusu ziara hiyo.

**Maandalizi**
Zoezi hili linaweza kufanyika tu wakati vijana wameshajua ni kampuni gani watakayotembelea. Wanaweza kuchagua kampuni hiyo katika zoezi 3.6 'Kupata kampuni kwa ajili ya ziara ya kiutafiti: Kwanini waende huko?' au katika zoezi 3.7 'Ni kampuni gani ninayohitaji kuitembelea?'.

**Maelezo**
'Maandalizi mazuri ni nusu ya mafanikio! Ikiwa umejiandaa vizuri kutembelea kampuni, una hakika kwamba utapata taarifa unayohitaji. Kama ilivyo muhimu kupata msaada kutoka katika familia yako au marafiki, ni vizuri wakajua unachoenda kufanya. Katika kipindi hiki, tunachanganya yale malengo mawili. Utajiandaa kutembelea kampuni yako kwa kuandika barua kwa wazazi wako/walezi/marafiki.'

**Utendaji**
1. Wape vijana kazi ya kuwaaandikia wazazi/walezi/marafiki zao barua kuhusu mpango wa kutembelea kampuni. Waambie wataje angalau mambo yafuatayo:
   - Ni kampuni ya aina gani unayoenda kuitembelea?
   - Je, wanazalisha/fanya/kuuza nini n.k?
   - Mna sababu gani ya jumla ya kutembelea kampuni hiyo? Kwanini ni muhimu?
   - Je, ni kipengele kipi mnahitaji taarifa zaidi? Kwa mfano: kazi wanazozitoa, soko, masharti ya kazi, mshahara n.k.
   - Kwanini kampuni hii mahsusi na fani hiyo?
   - Kwa namna gani unadhani vipaji na ujuzi wako unaendana na mazingira ya kazi?
   - Nimatarajio gani unayo kwa kutembelea kampuni hii?
   - Unatumaini kuona nini na kukupata uzoefu gani?
   - Ziara ya kampuni itachukua muda gani?
   - Utatembelea lini kampuni hii?
2. Waache washiriki wasome barua ya kila mmoja katika jozi na kutoa maoni kwa kila mmoja.
3. Waagize waandike barua kwa maelezo mazuri, wahusishe maoni ya wenzao katika kundi. Waruhusu wawape barua hizi wazazi au marafiki zao.
4. Watie moyo vijana kuwaomba wazazi wao, familia au marafiki kuwapa maoni na wao waoneshe mitazamo yao kwenye kipindi kinachofuata.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanavyojisikia kuhusu maandalizi ya namna hii ya kutembelea kampuni, wanapendezwa na nini? Je, palikuwepo na maswali yoyote magumu kujibu kuliko mengine? Je, vijana, baada ya kufanya kazi hii, bado wana maswali ambayo yanapaswa kujibiwa? Wanawezaje kupata jibu kwa maswali yao yaliyobaki? Wanajisikiaje kuruhusu wazazi, familia au marafiki zao kusoma barua zao? Je, wanasubiri kupata aina gani ya majibu? Je, vijana wanawafikiria wazazi wao, familia na marafiki wanaweza kuwa na masaada katika kukuza fani/kazi zao? Hakikisha unauliza majibu ya barua zao wakati wa kikao kijacho. Kivipi wazazi wao, familia zao, marafiki walipokeaje taarifa kuhusu ziara ya kampuni kwa namna hii? Walikuja na maoni yoyote mapya, mrejesho au msaada?

***Dondoo***
Zoezi hili linaweza pia kutolewa kama sehemu ya masomo ya Kiswahili, Kiingereza au mawasiliano. Hata hivyo, barua hii inawalenga wazazi/walezi/marafiki. Hii ina maana kwamba si barua rasmi. Katika barua isiyo rasmi lugha iwe kulingana na vijana wanavyozungumza na wazazi au marafiki zao.

**Uchunguzi wa kina**
Je, vijana wametunga wimbo za kufoka, wimbo, shairi, video fupi au barua pepe, badala ya barua za kawaida zinazohusisha taarifa zile zile.

# 3.10

# JIANDAE!

**Lengo**
Vijana wafanye maandalizi ya utendaji muhimu kwa ajili ya ziara kwenye kampuni.

**Maandalizi**
Fikiri mwenyewe juu ya majibu ya maswali utakayouliza. Je, hivi ndivyo unavyojiandaa unapoweka miadi? Weka maswali kwenye ubao kabla ya kipindi kuanza.

**Maelezo**
'Hivi punde utatembelea kampuni yako uliyochagua katika mazoezi yaliyopita. Kuwa na maandalizi mazuri ni muhimu pia. Itafaa kujibu maswali kadhaa kabla ya kwenda kuhakikisha kuwa hakuna jambo ambalo halitakupendeza.'

**Utendaji**
1. Lipatie kundi lako kazi ya kujibu maswali yafuatayo mmoja mmoja:
   - Ni wakati gani ninatarajia?
   - Niende na nini?
   - Nitasoma nini kabla?
   - Nitasafiri vipi kwenda kwenye kampuni?
   - Njia bora zaidi kwenda kwenye kampuni ni ipi?
   - Nitaambatana na nani kwenda huko?
   - Muda gani nitaondoka nyumbani?
   - Nitavaaje?
   - Namba ya simu ya kampuni ni ipi?
   - Jina na namba ya simu ya mtu atakayenipokea?
   - Nitajitambulishaje?
2. Waache waandike majibu yao katika madaftari yao na wayajadili baadaye darasani.

**Tafakuri**
Waulize vijana kama wanahisi wamejiandaa vizuri. Je, wana maswali mengine yaliyobaki? Ikiwa ndio, waache wapeane majibu juu ya maswali hayo. Watakie kila la kheri!

***Dondoo***
Angalia washiriki wako mmoja baada ya mwingine ili kuhakikisha kuwa wamejiandaa kikamilifu kwa ziara yao kwenye kampuni. Na kama kuna wenye wasiwasi unaweza kuwatia moyo. Unaweza pia kutoa kazi ya kutoa ripoti ya ziara yao.

# 3.11

# KUANGALIA NYUMA

**Lengo**
Vijana watafakari kama matarajio yao kwenye ziara yao ya kampuni yamefikiwa.

**Maandalizi**
Chukua sanduku la 'Kuangalia nyuma' na matarajio yote ambayo washiriki wameandika katika zoezi 3.4 'Kutarajia ziara ya kimafunzo'. Angalia kama maelezo yote ya vijana bado yapo katika sanduku?

**Maelezo**
'Umekuwa kwenye ziara ya kampuni na kabla ya hapo tulifanya zoezi 'Kutarajia ziara ya kimafunzo'. Umeandika kila ulilotarajia kutoka katika ziara hii. Sasa tutafanya zoezi la 'Kuangalia nyuma' na kila mtu atarejea alichoandika. Soma kwa sauti uliyoandika kwenye karatasi hiyo na ueleze ikiwa matarajio yako yamefikiwa. Toa maelezo.'

**Utendaji**
1. Jihadharini kwamba maelezo yote ambayo mnatarajia kwenye ziara ya kampuni yameandikwa, bado yapo kwenye chombo, kasha au bakuli.
2. Chukua maelezo moja wapo bila kuchagua na kumpa mshiriki aliyeandika.
3. Mshiriki ayasome kwa sauti.
4. Aelezee kama matarajio haya yametimizwa na aoneshe jibu.
5. Ikiwa ni lazima, watoe maelezo ya ziada.

**Tafakuri**
Waulize vijana endapo wanafikiri kwamba matarajio yao yalikuwa halisi na kueleza waliyojifunza juu ya kuweka matarajio.

***Dondoo***
Fanya zoezi hili kwa namna yoyote endapo umefanya pia zoezi 3.4 'Kutarajia ziara ya kimafunzo'.

# 3.12 MZUNGUKO

**Lengo**
Vijana watathmini ziara, matembezi yao kwenye makampuni waliyotembelea.

**Maandalizi**
Weka viti, bila meza, katika hali ambayo kuna mzunguko wa ndani na nje. Vijana walio kwenye mzunguko wa ndani wapangwe wakiwatazama wa mzunguko wa nje.

**Maelezo**
'Iwapo unapitia jambo fulani ni vyema ukalizungumza na kujifunza kwalo. Kwa kutafakari juu yake, utajifunza zaidi kupitia hilo. Wakati wa zoezi hili, tutazungumzia juu ya yale uliyoyaona wakati wa kutembelea makampuni. Katika awamu tano utachangia uzoefu wako na watu watano tofauti kwa kutumia mduara wa ndani na nje. Kila mzunguko uwe mara mbili na utumie muda wa dakika tatu; baada ya watu walio katika mduara wa ndani wasogee sehemu moja kushoto. Kila mshiriki achukue jukumu la msaili na msailiwa kwa mara tano.'

**Utendaji**
1. Washiriki katika mzunguko wa nje wawaulize maswali wale wa pembeni yao. Maswali yanashughulika na ziara ya kampuni. Baada ya dakika 3, wabadilishane majukumu na washiriki katika mahojiano ya ndani ya mduara na wale walio kwenye mduara wa nje.
2. Baada ya mzunguko mmoja mshiriki wa mzunguko wa ndani asogee kwenye kiti kingine cha kushoto. Sasa kila mtu ana mtu tofauti kwa mahojiano.
3. Tena, washiriki wahojiane kuhusu uzoefu wao wa kutembelea kampuni kwa muda wa dakika tatu. Baada ya mzunguko huu, washiriki wa mzunguko wa ndani wanasogea tena nafasi moja kushoto.
4. Rudia mpaka mizunguko mitano (5).

**Tafakuri**
Mizunguko itakapokuwa imekamilika, zungumzia changamoto ambazo vijana wamekabiliana nazo. Je, kuna maswali yoyote ambayo hayajaulizwa? Maswali yaliyo sahihi yalikuwa yapi? Je, vijana wanahisi ni kampuni ipi wangeenda kufanya mafunzo ya kazi?

***Dondoo***
Unaweza kusaidia vijana kwanza kwa kuonesha mfano wa jinsi ya kufanya mahojiano. Shiriki kwenye mzunguzo.

# 3.13 NIMESIMAMA WAPI?

**Lengo**
Vijana wapeane uzoefu wao kutokana na ziara ya kwenye kampuni na kutoa tathmini zao.

**Maandalizi**
Weka meza na viti pembeni na tengeneza sehemu ya wazi katikati ya chumba. Chora mstari katikati na kwa kutumia gundi ya karatasi. Kwa nusu moja, andika neno 'Kubali' na nusu nyingine neno 'Sikubali'. Unaweza pia kuandika 'Kubali' kwenye kipande cha karatasi na kwenye kipande kingine 'Sikubali' na na ning' iniza vipande hivyo viwili pande mbili tofauti za ukuta. Chapa au andika kauli zifuatazo. Bila shaka, uko huru kuongeza baadhi ya maelezo kwenye orodha hii:

- Nimejifunza mengi wakati wa ziara yangu kwenye kampuni.
- Nimegundua kazi ninayotaka katika siku zijazo.
- Bado nasita vile ninavyotaka kuwa.
- Nina ufahamu mzuri wa kazi yangu ya baadaye.
- Ziara yangu kwenye kampuni ilikuwa ya mafanikio makubwa.
- Nimeuliza maswali mengi wakati wa ziara yangu kwenye kampuni.
- Matarajio yangu yametimia.
- Ninajua nini cha kufanya baadaye.
- Napenda kufanya ziara nyingine kwenye kampuni.
- Napenda kufanya mafunzo yangu ya viwandani kwenye kampuni hii.

**Maelezo**
'Sasa na baadae ni muhimu kufahamu hali uliyo nayo sasa na unafikiria nini. Ikiwa hutatathmini hali yako, unaweza kwenda tu kwenye miduara bila kujifunza kutokana na uzoefu wako. Mstari wa katikati ni mstari wa kutenganisha kati ya 'Kubali' na 'Sikubali'. Utasikiliza maelezo kadhaa kuhusu matembezi uliyoyafanya kwenye kampuni. Ikiwa unakubaliana na kauli utaenda kwenye 'eneo la kukubali', ikiwa hukubaliana nenda kwenye, 'eneo la kutokubaliana'. Bila shaka, unaulizwa kuelezea zaidi kuhusu uchaguzi wako.'

**Utendaji**
1 Eleza tofauti kati ya maeneo mawili 'Kubali' na 'Sikubali'.
2 Ruhusu vijana kusikiliza maelezo moja baada ya jingine na baada ya kila taarifa kutolewa waache watembee kwenye eneo ambalo linahusiana na uzoefu wao.
3 Waulize wawili au watatu wao kwanini wamechagua upande mmoja au mwingine.
4 Endelea mpaka utakapokuwa na taarifa ya kutathmini na kutafakari juu ya uchaguzi uliofanywa.

**Tafakuri**
Liulize kundi ni aina gani ya mahitimisho yanayoweza kufikiwa baada ya wote 'Kubali' au 'Sikubali'. Ni nini kifanyike tofauti kwenye ziara nyingine za kampuni? Ni changamoto gani wanazoziona kwao wenyewe watakapotembelea kampuni nyingine?

***Dondoo***
Usishiriki katika majadiliano; waoneshe vijana matokeo ya chaguzi zao. Waulize watu wawili au watatu tu kuelezea kwa kifupi zaidi juu ya makubaliano yao au kutokubaliana na taarifa. Kumbuka kwamba utampa kila mtu nafasi ya kuelezea uchaguzi wake. Usiifanye kuwa ndefu sana, ikiwezekana harakisha.
Unaweza kuwauliza washiriki kutoa taarifa zao kuhusu ziara kwenye kampuni. Ongeza maelezo hayo kwenye zoezi na acha vijana pia waoneshe msimamo kwa 'Kubali' au 'Sikubali'.

# 3.14

# MAPITIO YA ZIARA

**Lengo**
Vijana watafakari ziara yao: Je, imekidhi matarajio yao?

**Maandalizi**
Kumbuka ni katika somo lipi ulipewa kazi ya kuchagua kampuni na kujiandaa kwa ajili ya ziara. Njia ipi uliyoitumia ili kuweka matarajio? Ni wapi vijana wanaweza kupata matokeo ya maandalizi hayo?

**Maelezo**
'Ikiwa tuna matarajio ya kupata kitu kabla hatujaingia katika utekelezaji, ni vyema kutazama nyuma baadae ili kuona kama matarajio yetu yametimia. Kwa njia hii, tunatambua kama matarajio yetu yalikuwa ya kweli au la. Na wakati huo huo, tunajua kama kuna matarajio ambayo yanahitaji kushughulikiwa.'

**Utendaji**
1 Wape vijana dakika chache kuandika maneno muhimu wanayopenda kuwauliza katika mapitio - wasilisho la dakika moja - kuhusu matarajio yao na uzoefu wao juu ya kutembelea kampuni.
2 Kila mshiriki aongee kwa dakika moja kuhusiana na uzoefu wao na matarajio yao ya kutembelea kampuni. Waombe waanze uwasilishaji wao kwa kusema: 'Ziara yangu kwenye kampuni ilikidhi' au 'Ziara yangu kwenye kampuni haikukidhi' matarajio yangu.
3 Baada ya kila pitio, kila mtu ajibu angalau maswali matatu kutoka kwa wanakikundi wengine.

**Tafakuri**
Liulize kundi ni aina gani ya hitimisho linaweza kutolewa kuhusu uhusiano kati ya matarajio na uzoefu halisi? Tunaweza kujifunza nini kutokana na hilo kwa ajili ya ziara na kutembelea kampuni nyingine? Ni matarajio yapi ambayo bado yanahitaji kuelezewa? Kwa nani? Jinsi gani ya kupanga hayo matarajio?

***Dondoo***
Weka umakini kwenye muda: weka kengele kwa wasilisho la dakika 1 tu. Hakikisha kwamba washiriki wanazungumzia matarajio waliyokuwa nayo kabla ya kutembelea kampuni. Waache wakumbuke mazoezi ya kipindi ambacho walishughulikia suala hilo.

**Uchunguzi wa kina**
Waruhusu vijana kutoa maelezo ya kina kwa picha, filamu, mahojiano n.k., maswali zaidi yanaweza kuulizwa na ratiba yako inatakiwa kurekebishwa. Wapatie washiriki muda mwingi zaidi.

# 3.15 Taswira ya siku ya kazi

**Lengo**
Vijana watafakari juu ya ziara yao kiubunifu.

**Maandalizi**
Unahitaji kujua ni makampuni gani washiriki wameyatembelea. Hakikisha kuwa kuna vifaa vya kutosha kutengeneza mfululizo wa michoro ya katuni: karatasi, picha, vifaa vya masoko, gundi, penseli, kalamu za wino mzito rangi tofauti, mkasi, kompyuta au laptop.

**Maelezo**
'Baada ya kutembelea kampuni huenda ukawa na hisia nzuri juu ya siku ya kazi za wastani. Katika kipindi hiki, utaonesha siku hiyo katika picha. Itakuwa ni mfululizo wa mchoro wa katuni, hadithi ndogo inayotolewa kwa picha. Wakati mwingine picha zinajieleza vizuri zaidi kuliko maneno. Aidha, mara nyingi ni nzuri, zinavutia au kufurahisha kuziangalia.'

**Utendaji**
1. Watake vijana kuelezea kwa maneno muhimu siku ya mfanyakazi katika kampuni waliyoitembelea. Waache wafanye kazi kwa jozi.
2. Waache kila mmoja akatafute picha zinazofaa, picha au michoro inayoonesha siku hiyo ya kazi.
3. Waombe waweke picha katika utaratibu ambapo shughuli mbalimbali zinazofanyika wakati wa mchana. Waache wafanye baadhi ya vipengele kwenye kipande cha karatasi.
4. Waache waweke picha zao za siku za kazi juu ya ukuta au juu ya meza na waache wachukue picha mchoro wao.
5. Kwa kuonesha matokeo kwa kila mmoja, waulize washiriki kuelezea nini na kwanini wamechora mchoro huu wa katuni. Usisahau kuwauliza ikiwa wangependa siku yao ya kazi kuonekana kama siku ya kwenye mchoro.

**Tafakuri**
Je, vijana wanaonaje ziara zao kwenye kampuni kwa mfumo huu? Je, waliona kitu chochote wakati wa kutengeneza mfululizo wa michoro ya katuni kilichowafanya watazame taaluma yao kwa njia tofauti? Je, kuna mambo mengine yoyote ambayo yamewapa ufahamu mpya juu ya kazi za kwenye kampuni hiyo?

***Dondoo***

Labda vijana wana matatizo katika kutengeneza mfululizo wa michoro ya katuni. Wahimize kuwa ni suala litakaloifanya ziara yao kwenye kampuni kuwa na maana. Haijalishi ubora wa katuni yao. Hakikisha kuwa kuna nafasi ya kutosha kwa kuonesha mfululizo wa michoro yote ya katuni, ili vijana waweze kuona kazi ya kila mmoja.

# 3.16

# TATHMINI NA SHUKURANI

KARATASI YA ZOEZI 3.16

**Lengo**
Vijana watathmini ziara yao ya mafunzo kwenye kampuni kwa kutuma barua ya tafakuri na shukurani kwa msimamizi/mkufunzi wa kampuni hiyo.

**Maandalizi**
Toa nakala yenye maswali ya tathmini kwenye karatasi ya zoezi 3.16 'Tathmini ya ziara kwenye kampuni' kwa kila mshiriki. Hakikisha kuwa unajua ziara ngapi zimefanyika kwenye kampuni, na zimefanywa na nani, jina la kampuni na msimamizi/mkufunzi. Ikiwa kundi zima lilitembelea kampuni hiyo hiyo barua moja ya shukurani inatosha. Vinginevyo barua nyingi za shukurani zinahitajika.

**Maelezo**
'Mtandao pia humaanisha kuwashukuru wengine kwa walichokutendea. Katika kazi hii, utajaribu kutathmini matembezi yako kwenye kampuni. Ndani ya wiki mbili tutatuma ujumbe wa 'shukurani' pamoja na fomu za tathmini kwa mkufunzi wa kampuni. Tathmini ni muhimu sana, si tu kwetu wenyewe, lakini pia kwa msimamizi/mkufunzi wa kampuni. Kwa njia hii, tunamwonesha yale tuliyoyapenda na yapi wayafanyie marekebisho wakati mwingine.'

**Utendaji**
1. Omba kundi lako kujaza fomu ya tathmini kwenye karatasi ya zoezi namba 3.16 'Tathmini ya ziara kwenye kampuni'. Kuwa kamili kama iwezekanavyo. Wajulishe mapema kuwa msimamizi/mkufunzi atasoma fomu ya tathmini kwa umakini.
2. Waulize washiriki ambao wana muda wa ziada kuandaa mfano wa barua ya shukurani kwa msimamizi/mkufunzi.
3. Wawasilishe rasimu ya barua zao za shukurani na kuzijadili kwenye kundi: Je, kuna maoni au mabadiliko muhimu ya kuongeza katika barua hizo? Wakati barua iko tayari, isome tena kwa kila mmoja kisha andika barua mpya.
4. Tuma fomu za tathmini na barua ya 'shukurani' kwa msimamizi/mkufunzi ndani ya wiki mbili baada ya kutembelea kampuni.

**Tafakuri**
Tathmini na kuzungumzia juu ya mazuri na madhaifu yaliyopatikana katika ziara ya kwenye kampuni. Shirikisha maoni yako kuhusu majibu yaliyotolewa kwenye fomu za tathmini. Je, kuna maboresho yoyote ambayo yanaweza kufanywa katika ziara ya kwenye kampuni hii kuwa yenye thamani zaidi? Waulize washiriki kama wangependa kufanya kazi katika kampuni hiyo baadae? Je, walikutana na watu ambao wangependa kuwaongeza kwenye mtandao wao? Kwanini? Wanataka kuwasiliana na watu hao kwa njia gani?

***Dondoo***

Onesha kwamba zoezi hili linalenga kutia mkazo kwenye vipengele muhimu katika ziara ya kwenye kampuni. Bila shaka, ukosoaji wa kujenga unaweza kufanywa, lakini hakikisha mnawasilisha kama mawazo ya kuboresha. Uimarishaji chanya wa uzoefu ni wa thamani zaidi kwa kila mtu.
Kusanya tathmini zote za ziara za kwenye kampuni, zitakusaidia kujenga mtandao mzuri wa taasisi yako. Mtandao huu ni muhimu sana unapotaka kutoa CBET (Mafunzo na Elimu ya Kuzingatia Umahiri), mbinu ya mafundisho inayoitikia matakwa ya soko la ajira.
Bila shaka, ingefaa zaidi kama kila mshiriki aandike barua yake ya 'shukurani' kwa msimamizi/mkufunzi. Ni suala binafsi na bora kwa kujenga uhusiano wa karibu. Barua ya shukurani inaweza kuandikwa kwa msaada wa walimu wa Kiswahili au Kiingereza.

## 3.17 DAIMA UNAJIFUNZA JAMBO

**Lengo**
Vijana watafakari juu ya vipengele vya fani wanayoipenda zaidi na wasiyoipenda.

**Maandalizi**
Inafaa kujua ni makampuni gani yaliyotembelewa na vijana na kwa sababu gani. Unaweza kuuliza maswali yenye maana zaidi katika suala hilo. Hakikisha una karatasi za kutosha za A4 au ruhusu vijana kutumia madaftari yao 'kazi yangu'.

**Maelezo**
'Bila shaka, ni vyema kuwa na kazi ambayo daima unaweza kufanya mambo yanayokufaa. Lakini hili linawezekana kila mara? Unafikiria nini? Kwa kiasi kikubwa baadhi ya vipengele vya kazi vinakufaa wewe na vingine havikufai. Mambo hayo huja na kazi. Hilo ndiyo tutakalokuchunguza katika zoezi hili. Tutaangalia tena kwenye ziara yako ya kwenye kampuni na tutaangalia upya kile ulichopenda na ambacho hukukipenda sana.'

**Utendaji**
1. Wape washiriki wote kipande cha karatasi cha A4 tupu au wafanye kazi kwenye madaftari yao.
2. Karatasi lazima zigawanywe katika sehemu mbili. Nusu moja, mshiriki aandike maneno 'Fani/kazi inayonifaa' na nusu nyingine 'Fani/kazi isiyonifaa'. Watoe majibu yao wakirejea kwenye taaluma au kazi walizoangalia kipindi cha ziara yao kwenye kampuni.
3. Wafanye waandike vitu vingi vinavyokuja akilini mwao. Usiwape muda mwingi wa kufikiria. Daima wanaweza kufuta vitu baadaye. Fikiria vitu kama: Saa za kazi, jamaa, utaratibu, likizo, ratiba n.k.
4. Katika jozi, washiriki wabadilishane karatasi zao na kutoa mrejesho kwenye orodha za kila mmoja. Waache wajadili umuhimu wa tafiti zao kwa ajili ya mipango yao ya kazi.
5. Mwisho, waombe watoe hitimisho binafsi.

**Tafakuri**
Waulize vijana yale waliyojadiliana katika jozi na yapi mahitimisho binafsi waliyotoa. Je, wanataka kusema nini kwenye hitimisho hilo? Je uchunguzi au uzoefu unahitajika zaidi? Je, ni vidokezo gani vinaweza kutolewa?

***Dondoo***
Kazi hii inalenga kuwafanya vijana kujua kwamba, baada ya kufanya uchaguzi kwa mafunzo fulani au kazi, si kila kitu kitafanikiwa. Lazima iwepo aina ya usawa kati ya taswira chanya na hasi za kazi ya baadaye. Wakati mwingine kuna haja ya kufanya chaguo: ama kuendelea na mafunzo kwa aina hii ya taaluma au kuhamia fani nyingine. Panga miadi na washiriki kwa mfumo wa mtu mmoja mmoja, kama hakuna usawa.

**Uchunguzi wa kina**
Andaa orodha ya mada ambazo zinaonekana kuwafaa au kutowafaa vijana. Linganisha na maadili ya kazi ambayo unaweza kuyapata katika zoezi 2.9 'Maadili yangu makuu ya kazi '. Kabla haujafanya zoezi hili, fanya tu katika somo linalofuata. Wakati mwingine pia husaidia wakati unapomkaribisha mtu ambaye ameshughulikana na shida hizo yeye mwenyewe na kumwuliza mtu huyo jinsi alivyoweza kuachana na mambo yasiyofaa zaidi.

3.18

# KUTAFUTA KAMPUNI KWA AJILI YA MAFUNZO YA VIWANDANI

**Lengo**
Vijana waanze kwa kuangalia kampuni ambayo wanaweza kufanya mafunzo yao ya viwandani, kwa kuzingatia mahitaji ya programu ya mafunzo ya ufundi, mitihani na mahitaji yao wenyewe.

**Maandalizi**
Panga darasa katika hali ambayo washiriki wanaweza kufanya kazi katika vikundi vya watu watatu au wanne. Ingawa unatarajia wanafunzi wawe na uwezo wa kuchagua kampuni wenyewe, ni muhimu pia kuwa na majina ya makampuni ambayo wanafunzi wengine wamepata sehemu nzuri kwa ajili ya kazi inayohitaji mafunzo. Weka makampuni hayo kama sehemu ya kimbilio kwa wanafunzi ambao hawawezi kupata kampuni yao wenyewe. Angalia kama taarifa nzuri na vipeperushi vinapatikana. Kompyuta mpakato, simu maizi na intaneti nzuri ni muhimu pia.

**Maelezo**
'Kujifunza kwa utendaji. Kwa kuweka uzoefu katika utendaji kwenye kampuni, utajifunza mengi. Kwa kufanya kazi katika mazingira halisi, unapata maarifa, ujuzi na mtazamo unaohitaji katika fani au kazi yako ya baadaye. Lazima ufanyie mambo. Na kwa kufanya kazi za kitaaluma, unajifunza unachopenda au usichopenda, vipaji vyako ni vipi na ni vitu gani bado unapaswa kujifunza. Nenda kafute kampuni ambapo unaweza kujiandaa kwa njia sahihi ya kazi yako ya baadaye.'

**Utendaji**
1. Waagize vijana kuandika vigezo watakavyotumia kuchagua kampuni inayowafaa. Inapaswa kuwapa nini? Wanataka kufanya kazi gani? Wanataka kujifunza nini?
2. Toa taarifa shuleni kuhusu mahitaji ya kampuni ili kutoa mafunzo sahihi ya viwandani. Kwa vipi mafunzo ya viwandani yanalingana na mtaala, mipango ya kujifunza na sheria za mitihani? Ni aina gani ya miongozo lazima kampuni itoe kwa vijana? Na nani katika shule atawasimamia wakati wa mafunzo ya viwandani?
3. Ligawanye kundi katika makundi ya wanafunzi watatu au wanne.
4. Omba vikundi vidogo vijadili mahitaji ambayo kampuni inatakiwa kuwa nayo; ni aina gani ya shughuli, kazi ambazo wanataka kuzifanya wakati wa mafunzo yao ya viwandani ili kujifunza zaidi na jinsi gani hili litasaidia kuwa tayari kwa ajili ya mitihani yao baadaye?
5. Litake kundi hili kuangalia angalau makampuni matatu ambayo yanaweza kukidhi mahitaji yao. Kuyapata, wanaweza kutumia mtandao wao wenyewe, vipeperushi vyote vinavyopatikana kwenye mtandao.
6. Waruhusu waandike taarifa zote sahihi walizopata kuhusiana na makampuni hayo, kuonesha kwanini wanafikiri kuwa kampuni hii itatoa nafasi nzuri kwa ajili ya mafunzo ya viwandani.
7. Agiza kila kikundi kidogo kuwasilisha makampuni matatu waliyochagua na watoe sifa kwanini wameyachagua.
8. Toa nafasi kwa mwanafunzi mwingine kuuliza swali moja au mawili baada ya kila wasilisho kuhusu makampuni matatu yaliyochaguliwa. Wanaweza pia kutoa maoni juu ya kile wanachopenda kuhusu makampuni.

**Tafakuri**
Waulize wanafunzi wanafikiria nini juu ya zoezi hili kama hatua ya kwanza ya kupata kampuni inayofaa. Je, wameweza kukusanya taarifa za kutosha? Nini kingine wanahitaji kupata mahali sahihi pa mafunzo ya viwandani? Je, ni hatua gani zitafuata? Tenga muda wa kuzungumza juu ya hili katika somo linalofuata. Toa msaada kwa mmoja mmoja au katika vikundi vidogo.

***Dondoo***
Kama mkufunzi hakikisha kwamba una taarifa zote unazohitaji: Je, mwanafunzi huyo anahitaji kujifunza nini kulingana na mtaala na mitihani na ni vigezo gani kampuni inatakiwa kuwa navyo? Unahitaji kujua vigezo vyote vya Kituo chako cha Mafunzo ya ufundi, VTA, VETA au NACTE. Inaweza kuwa kazi ngumu kwa wanafunzi. Je, wamejadili mapema vigezo vya uwekaji mzuri? Je, wanajua hasa nini wanahitaji kujifunza? Ikiwa mambo hayo hayatakuwa wazi kwao, inaweza kuwa vigumu kupata kampuni inayofaa. Kwa hiyo, toa msaada iwezekanavyo kwa wanafunzi wako, endelea kuomba ufafanuzi na hoja. Wahimize wanafunzi kupata majibu ya maswali yao wenyewe.

**Uchunguzi wa kina**
Waalike wanafunzi kutoka miaka iliyopita ili kuzungumza juu ya uzoefu wao wa mafunzo ya viwanda. Wawape wanafunzi wako vidokezo na maelezo na juu ya maswali kama: Je, hali ya hewa ni muhimu mahali pa kazi? Ni vigezo gani vinatakiwa kwa makampuni ambapo wanafunzi wanaweza kujifunza mengi? Njia bora zaidi za kukabiliana na kampuni ni zipi?

# 3.19 MAHOJIANO YANGU YA KWANZA NA KAMPUNI YA MAFUNZO YA VIWANDANI

**Lengo**
Vijana wajiandae kuwasiliana na kampuni waliyoichagua kwa ajili ya mafunzo ya viwandani.

**Maandalizi**
Hakikisha kuwa umejiandaa vizuri, tayari umefikiri juu ya maswali na majibu, kwamba unaweza kuwasaidia wanafunzi wako. Hakikisha una maswali katika orodha ambayo yanaweza kuonekana kwenye ubao au unayo kwenye karatasi.

**Maelezo**
'Sasa umepata kampuni ambayo ungependa kufanya mafunzo yako ya viwandani, unahitaji kupanga kwanza kuwasili mara ya kwanza kwenye kampuni. Huu ni wakati muhimu. Hakikisha unaonekana vizuri ikiwa umealikwa kwa mahojiano. Je, unaonekanaje wakati wa mahojiano? Je, unataka kujua nini kuhusu mwongozo ambao hutolewa katika kampuni hii? Kwa kadri ulivyojiandaa zaidi, unakuwa kwenye nafasi nzuri ya kukubalika na kampuni kufanya mafunzo yako ya viwandani.'

**Utendaji**
1. Ligawanye kundi katika makundi matatu.
2. Vijana wajadili maswali yafuatayo kwa pamoja:
   - Njia bora zaidi ya kuwasiliana na kampuni ni ipi?
   - Ni maswali gani ambayo yanapaswa kuulizwa kwanza?
   - Ni lipi ungependa zaidi kulijua?
   - Jinsi unavyopaswa kuonekana wakati umekaribishwa kwenye mahojiano?
   - Uvae namna gani?
   - Nini cha kusema wakati unapoingia?
   - Ikiwa kuna mapokezi, unaweza kujitambulishaje?
   - Kuhusu mikataba ya kufanya kazi, mfano, saa za kazi, matumizi ya simu yako ya mkononi, mwalimu, sikukuu, upungufu wa chakula cha mchana, ugonjwa, posho, usafiri, nguo za kazi n.k .
   - Unataka kujifunza nini wakati wa mafunzo yako ya viwandani?
   - Ni taarifa gani kuhusu mahitaji ya shule unaweza kuipatia kampuni? Kama vile idadi ya masaa ya mafunzo, idadi ya wiki, idadi ya siku kwa wiki, matarajio ya mafunzo na mambo mengine muhimu ambayo kampuni inapaswa kujua kuhusu wewe.
3. Waelekeze vijana kuandika mambo muhimu zaidi katika madaftari yao ili wasiyasahau.

**Tafakuri**
Waombe vijana washirikishe maandalizi yao. Ni vidokezo gani ambavyo vinaweza kutolewa kwa makundi mengine? Je, waligundua nini kuhusu wao wenyewe wakati wa kufanya zoezi hilo? Ni msaada gani zaidi wanaohitaji? Wapi na jinsi ya kuupata?

***Dondoo***

Jaribu kuweka wazi kuwa kuna nafasi moja tu ya kuufanya muonekano wako wa kwanza kuwa wa kuvutia. Fanya zoezi 'Jinsi ya kujitambulisha kwenye usaili' katika mchezo wa kuigiza. Unaweza kutumia mazoezi kutoka kwenye mada ya 4 ' Gundua mtandao wako' na mada ya 6 'Mpango kazi wako na kuomba kazi'.

**Uchunguzi wa kina**
Waalike wanafunzi kutoka miaka ya nyuma kuwaambia wanakikundi wako kuhusu uzoefu wao na mafunzo ya viwandani. Kuna ushauri gani mzuri wa kutoa? Je, ni nguo gani za kuvaa. Jinsi ya kuwa na mazungumzo mazuri kwa mara ya kwanza kutembelea au kupiga simu? Jinsi ya kujiandaa kwa njia bora zaidi? Walipenda au hawakupenda nini wakati wa usaili wao wa kwanza?

# 3.20 HISIA YANGU YA KWANZA KWENYE MAFUNZO YANGU YA VIWANDANI

**Lengo**
Baada ya wiki moja au mbili, baada mafunzo ya viwandani vijana watafakari juu ya uzoefu wao wa kwanza.

**Maandalizi**
Hakikisha unafahamu makampuni ambayo wanafunzi wako watafanyia mafunzo yao ya viwandani. Weka viti na meza kuruhusu wanafunzi kufanya kazi katika kundi la watu watatu. Angalia kama maswali yanaonekana kwenye ubao au tengeneza karatasi yako mwenyewe kwa njia ambayo wanafunzi wanaweza kuandika majibu yao kwenye karatasi hiyo ya zaoezi.

**Maelezo**
'Kusudi la mafunzo ya kazi ni kujifunza zaidi juu ya taaluma yako ya baadae na kujifunza nini unatarajia. Lengo la zoezi hili ni kutoa maana kwa kila kitu ulichojifunza wakati wa mafunzo yako kwa kurejea wakati uliopita. Kwa maneno mengine: kwa kutafakari juu ya uzoefu wako, utajifunza zaidi kuhusu kazi yako na kuhusu wewe mwenyewe.'

**Utendaji**
1. Watake vijana kila mmoja kutafakari juu ya maswali yafuatayo na kuandika mawazo yao:
   - Je, umejisikia kukaribishwa katika eneo lako la mafunzo ya viwandani? Ikiwa ndiyo au hapana, ni kwa sababu gani?
   - Nini mawazo yako ya kwanza ulipoona jengo la kufanyia kazi?
   - Je, ulipata ziara? Je, ni yapi mawazo yako kuhusu eneo hilo?
   - Je, kuna mgahawa? Umeupenda? Unaonekanaje?
   - Je, umetambulishwa kwa wafanyakazi wengine? Kwa njia gani na ulipenda hivyo?
   - Umeyaonaje mazingira ya kazi katika kampuni? Je, ni mazuri, unajisikia vizuri?
   - Vipi kuhusu jina la kampuni? Je, ni sahihi kulingana na wewe? Kwanini? Kwanini isiwe?
   - Upi ulikuwa mtazamo wako wa kwanza juu ya msimamizi wako/mkufunzi?
   - Je, umeweza kuuliza kila kitu? Imekuwaje? Ni nini kilichokufanya uulize kila kitu ulichotaka? Na ikiwa sio, ni sababu gani?
   - Je, umetakiwa kufanya kazi tayari? Ikiwa ndivyo, ulifanya nini? Ikiwa sio, unaanza kufanya kazi lini?
   - Waulize washiriki kutoa alama kutoka 1 hadi 10 kwa mambo yafuatayo:
     - Najihisi salama na kukubalika
     - Wakati wa mafunzo haya ya viwandani, ninaweza kujifunza mengi
     - Najisikia huru niwapo na wafanyakazi wenzangu
     - Nitapata msaada mzuri wakati nitakapouhitaji
2. Ligawanye kundi katika makundi matatu.
3. Waelekeze washiriki kuzungumza kuhusu alama walizotoa katika vipengele hivyo vinne. Kwanini walitoa alama hiyo? Waelekeze wabadilishane mawazo juu ya hilo.
4. Waombe wakamilishe sentensi zifuatazo za wanakikundi wenzao wawili: 'Kwa wiki ijayo, kama ningekuwa wewe na kama ningekuwa nafanya kazi kwenye eneo hili la mafunzo ya viwandani, ninge .................... '.
5. Washiriki wote waaandike vidokezo viwili walivyopata.

**Tafakuri**
Uliza vidokezo viwili ambavyo kila mshiriki amepata kutoka katika vikundi vya wenzao, wakati walipotakiwa kukamilisha sentensi. Je, vidokezo hivyo vimejikita katika uzoefu upi? Je, vidokezo vina msaada kiasi gani? Je, ni kitu gani wangefanya tofauti wakati mwingine?, au watafanya hivyo hivyo, kwanini? Je, kuna kitu ambacho wanahitaji kuzungumza na msimamizi/mkufunzi wa kampuni?

***Dondoo***

Katika kazi hii, vijana wanapewa changamoto kueleza mawazo yao ya kweli na hisia kuhusu mafunzo ya viwandani. Sisitiza kuwa hakuna majibu 'yasiyo sahihi'; ikiwa wamepata kitu kwa namna moja au nyingine, ni sawa. Kwa kulizungumzia wataweza kujifunza maana yake. Wanajifunza juu yao wenyewe, ambayo ni kigezo cha kufanya mabadiliko. Kila kitu kitakuwa sawa ikiwa watakuwa waaminifu juu yao wenyewe, hata kama mambo hayataenda kama walivyopanga.

**Uchunguzi wa kina**
Hamasisha vijana kuweka miadi ya kuzungumza na msimamizi/mkufunzi wao kutoka kwenye kampuni ili kubadilishana mawazo. Mkufunzi anahitaji kuwa sehemu ya mchakato wa kujifunza. Kwa njia hii, atajifunza zaidi juu ya wanafunzi wake kwenye mafunzo ya viwandani na ataweza kuwaongoza kwa njia inayofaa zaidi.

# 3.21 NINA USTADI WA KUTOSHA?

**Lengo**
Vijana wabadilishane changamoto ambazo wanaweza kukutana nazo kazini na kujadili njia tofauti za kukabiliana nazo.

**Maandalizi**
Weka viti katika mduara bila meza. Ikiwezekana, unaweza kuongeza baadhi ya uzoefu wako mwenyewe wa kushughulikia changamoto wakati wa kazi yako kama mkufunzi. Fikiria changamoto zote na jinsi unavyoweza kuzitatua na jinsi zinavyohusiana na maadili yako.

**Maelezo**
'Kila mtu atakutana na ugumu na hali ya kazi kama vile: 'Kitu hakiendi jinsi inavyotakiwa, lakini sijui jinsi ya kushughulikia'. Labda ikatokea kwamba kiongozi wa kampuni anauliza unaendeleaje. Unasita endapo unaweza kumwambia mambo ambayo hayaendi vizuri au hukubaliani nayo. Unafikiria 'Ninaweza kumwambia? Je, ninaruhusiwa kufanya hivyo?' Au ninaweza kumwambia wale wenzetu waliopiga simu wakiwa wagonjwa, wote sio wagonjwa kabisa, wakati bosi ananiulizia mambo yakoje? Katika zoezi hili, tutazungumzia kuhusu masuala hayo na jinsi ya kukabiliana nayo.'

**Utendaji**
1. Waambie vijana wanaenda kujadili hali kadhaa ambazo zinazoweza kutokea kazini, ambayo si rahisi kupata utatuzi. Zinaitwa changamoto. Kila mtu anajua kuna kitu hakiendi sawia, lakini inategemea hali na watu wanaohusika jinsi ya kukabiliana na hali hiyo.
2. Angalau zungumzia hali mbili kati ya hali zifuatazo katika kundi zima au katika vikundi vya watu 8 hivi:
   - Ninapata kazi ngumu kutoka kwa kiongozi wangu. Hilo hutokea mara kwa mara. Sijui kabisa anachotaka, lakini ninaogopa kumuuliza. Aidha, najua kuwa meneja wangu anataka kwenda kwenye mkutano mgumu katika muda wa dakika 10 na ninaona ana hofu juu yake. Nini cha kufanya?
   - Meneja wangu ana hasira kidogo kwa sababu ya kazi yangu. Na yuko sahihi, lakini hajui kwamba wazazi wangu wanakaribia kutengana. Ni vigumu kwangu na sijamwambia. Nini cha kufanya?
   - Ikiwa mtoto wangu anaumwa, nitakaa nyumbani ili kumhudumia. Katika hali hiyo, nitamwambia bosi wangu kwamba ninaumwa. Hii inamaanisha kuwa wenzangu watafanya sehemu ya kazi zangu. Baadhi ya wenzangu wanajua kwamba mimi si mgonjwa. Nini cha kufanya? Nimemuomba bosi wangu kufanya kazi siku 4 kwa wiki, ili nisiseme uongo endapo nikibaki nyumbani. Hakubali.
   - Ikiwa meneja wangu anakuja kwenye meza yangu, ninabadilisha haraka picha kwenye kompyuta yangu kwa sababu nilikuwa nikiangalia habari au 'Twitter', au 'linkedIn' na hii haikubaliki kazini. Nini cha kufanya?
   - Idara nzima inajua kwamba mwenzao amefanya kosa kubwa. Msimamizi hana ujasiri wa kumwambia kiongozi wake. Sisi sote tunaelewa hilo. Nini cha kufanya?
   - Asubuhi moja, nyaya za kompyuta zetu zote zimekatwa. Hakuna dalili za uhalifu au uvamizi. Kiongozi anatoa vidokezo kwamba anajua kuwa mmoja wa wafanyakazi wenzetu anahusika. Nini cha kufanya?
   - Mwenzangu amebadili muda wa kufanya kazi na mimi bila mimi kujua. Sasa ni lazima kufanya kazi jioni hii na nina mipango ya kuogelea na marafiki zangu. Nini cha kufanya?
   - Mwenzangu kapiga simu anaumwa. Lakini nilipokuwa mjini nilimwona akinunua vitu na mwanawe. Nini cha kufanya?
3. Kila baada ya changamoto kujadiliwa, waagize vijana kufupisha mambo muhimu yanayosababisha changamoto hizo. Hii husaidia kutoa mwanga juu ya kupima faida na hasara. Baada ya hayo, waulize nini kinachoonekana kuwa njia bora ya kukabiliana na hali hiyo.

**Tafakuri**
Je, kijana huyo amejisikiaje kuzungumzia changamoto zake? Je, wamezitambua hali hizo ngumu katika maisha yao? Walijifunza nini kutoka kwenye mjadala? Waache waeleze uhalisia wa majadiliano hayo.

***Dondoo***
Kuzungumzia kuhusu shida hizi kunaweza kufanyika pamoja na washiriki wote kwa wakati mmoja au kwenye makundi ya watu 6 hadi 8. Unapoamua kuzungumza katika vikundi vidogo, Ni jambo jema kumteua mwenyekiti atakaye endesha majadiliano kwa utaratibu. Kila mtu anapaswa kuwa na muda wa kumwambia kila kitu anachotaka. Watu wakimya wanapaswa kuruhusiwa kusema pia.
Jaribu kujenga mazingira mazuri wakati wa majadiliano. Wafanye wajifunze kwamba hakuna njia rahisi ya kutoka. Kila kitu kina historia yake, na sio sawa kusema kwamba kuna suluhisho moja kwa kila kitu, kwa sababu haipo. Sio rahisi na kuna sababu nyingi zaidi na hoja ambazo unaweza kufikiria. Jihadharini na hili. Usiseme kamwe: 'hili ndilo suluhisho moja pekee', kwa sababu si kweli. Jaribu kutaja uzoefu ulioshudia mwenyewe.

**Uchunguzi wa kina**
Athari ya kuzungumzia changamoto huongezeka wakati vijana wanapozungumzia kuhusu hali ambazo wamezipitia. Kwanza, waulize vijana kuangalia 'nini', 'nani' na 'kwanini' ya changamoto zao. Majibu na utatuzi utakuja baadaye.

3.22

# BARUA YANGU KUHUSU UZOEFU WANGU WAKATI WA MAFUNZO NDANI YA KAMPUNI

**Lengo**
Vijana watafakari juu ya uzoefu wao wa mafunzo ndani ya kampuni katika wiki zilizopita.

**Maandalizi**
Weka meza katika umbo -U ili kuhakikisha kwamba vijana wanaweza kutazamana. Hakikisha kwamba maswali yameandikwa kwenye ubao.

**Maelezo**
'Lengo la mafunzo yako ya viwandani ni kujifunza juu ya fani yako ya baadaye na kujifunza nini unatarajia. Hata hivyo, lengo la mafunzo ya kazi pia ni kutoa maana kwa yote uliyopitia. Kwa maneno mengine: kwa kujadili uzoefu wako na kwa kuyazungumzia na wengine, utajifunza zaidi kuhusu wewe mwenyewe, mtazamo wako mwenyewe wa kazi na jinsi ya kufanya kama mtaalamu.'

**Utendaji**
1 Waelekeze vijana kuandika barua ambayo kwayo wanatathmini uzoefu wao wakati wa mafunzo yao ya viwandani ya wiki iliyopita. Wape fursa ya kuchagua nani wanataka kumwandikia: mwalimu, wazazi wao, marafiki, wanafamilia wengine. Barua hiyo inapaswa kuanza na: Hallo ......, wiki iliyopita nilifanya mazoezi yangu ya utendaji. Katika barua hii, napenda kukuambia kuhusu uzoefu wangu.
2 Waelekeze kuandika kuhusu mada zifuatazo:
- Nilifanya nini wiki iliyopita?
- Nini kilikuwa kipya kabisa kwangu?
- Nini kilinivutia zaidi kufanya katika kipindi hiki cha mafunzo. Kwanini?
- Akina nani wenzangu wenye uzoefu wanaofanya kitu ambacho ningependa kujifunza pia?
- Je, msimamizi/mkufunzi wangu alinisaidia vizuri? Kwanini nadhani hivyo?
- Ni nini kilikuwa kigumu kwangu wiki hii? Nini kilitokea? Nimejadiliana hili na msimamizi wangu/mkufunzi? Mazungumzo haya yameendaje? Tuliweza kupata suluhisho?
- Ni nini kingine cha kusema ambacho sijakitaja?

3 Hakikisha vijana wanazituma barua zao (kwenye karatasi au kwa njia za kisasa kidijitali). Waelekeze wamwombe mpokeaji kuwajibu au waombe mazungumzo madogo kuhusu hilo.

**Tafakuri**
Waelekeze washiriki wachache kuzisoma barua zao kwa sauti. Walipata nini? Ilikuwaje kupima uzoefu wa mafunzo kwa njia hii? Je, walipata kitu ambacho hawakukitegemea kabla? Je, msimamizi/mkufunzi anahitaji kujua kuhusu hili?

***Dondoo***
Wahamasishe vijana waandike barua kwa mtu waliyechagua. Hii pia ina maana kwamba wanahitaji kurekebisha mtindo wao wa kuandika kwa aina ya mpokeaji. Je, ni sahihi kutumia lugha ya mitaani au ni bora kuandika barua rasmi zaidi? Labda mwalimu wa Kiingereza, Kiswahili au Mawasiliano anaweza kukusaidia kukushauri kuhusu lugha sahihi. Ikiwa muda wa kumaliza barua hautoshi kwenye kipindi kimoja, fanya kama kazi ya nyumbani. Waelekeze washiriki kuleta nakala ya barua yao kwenye kipindi kingine cha tafakuri.

3.23

# PICHA ZINAZOWAKILISHA MAFUNZO YANGU NDANI YA KAMPUNI

**Lengo**
Vijana waoneshe siku ya kazi inaonekaje na ni kipi wanakipenda sana au kukipenda kidogo.

**Maandalizi**
Panga darasa kwa hali ambayo vijana wana nafasi ya kutosha ya kufanya kazi. Meza zinaweza kuwekwa pamoja katika kundi la watu wanne. Angalia kuwa kuna nyenzo za kutosha za kufanya kazi hii: vipeperushi, magazeti, majarida, zana za asili, gundi, mkasi, kompyuta na intaneti nzuri, mashine ya kupigia chapa n.k.

**Maelezo**
'Picha zinasema zenyewe; wakati mwingine ni muhimu kuliko maneno. Katika kazi hii, tutaona kama ni kweli. Utaelezea kwa njia ya picha siku yako ya kawaida katika mafunzo yako ya viwandani, ikiwa ni pamoja na kile unachopenda na usichokipenda.'

**Utendaji**
1. Waelekeze vijana kuandika mmoja mmoja namna siku yao ya kawaida kazini inavyokuwa. Walipenda nini? Hawakupenda nini?
2. Wakusanye picha au taswira na michoro ili kuangalia siku ya kazi: kwenye mtandao, katika magazeti au katika vitu vya asili.
3. Wakusanye kila kitu walichonacho.
4. Wakiweke walichokikusanya kwenye ukuta au wakioneshe kupitia projekta.
5. Waelekeze vijana kuchukua picha ya matokeo yao.
6. Waelekeze vijana kuelezea vitu walivyokusanya.

**Tafakuri**
Jadili mikusanyiko ya picha. Zipi ni tofauti. Upi ni mfanano? Wamefanya uvumbuzi gani katika zoezi hili? Kuna vitu ambavyo walikuwa hawajagundua? Wangependa kufanya tathmini kwa namna gani katika mafunzo ya kazi kwa namna hii?

***Dondoo***
Kama mkufunzi, ni muhimu kuifanya kazi hiyo mwenyewe kwanza. Hii husaidia kuwa mfano mzuri na unaweza kujibu maswali yao vizuri. Wanaweza pia kutambua kuwa mkufunzi wao hapendi kila kitu kuhusu kazi yake na wataona kwamba hii ni ya kawaida.

# 3.24

# STARR–MBINU YA KUTOA MAANA YA UZOEFU

KARATASI YA ZOEZI 3.24

**Lengo**
Vijana watafakari juu ya tukio ambalo lilikuwa muhimu kwao wakati wa mafunzo yao ya viwandani na ambalo walitumia vipaji na ujuzi wao. Wanajifunza kutoa maana ya uzoefu huo.

**Maandalizi**
Panga meza katika hali ambayo vijana wataweza kufanya kazi katika kundi la watu watatu. Kama mkufunzi, unahitaji kujua njia ya STARR. Hapo ndipo unaweza kujibu maswali kutoka kwa vijana na kuwasaidia wakati wao wanapokwama. Kwa hiyo, fanyia mazoezi njia hii na wenzako au marafiki. Andaa karatasi ya zoezi 3.24 'STARR-njia ya kutoa maana ya uzoefu'.

**Maelezo**
'Wakati wa mafunzo yako ya viwandani kuna kitu ambacho hutokea ambacho ni muhimu kwako. Kwa njia ya STARR, unaweza kutafakari juu ya shughuli zako na kujifunza kutoka kwayo. Kwa kujibu maswali mengi, unajifunza kuelezea hali, kazi yako, matendo yako na nini matokeo ya utendaji wako. Mwishoni unatoa tafakuri ya mwisho. Unafanya kazi katika kikundi cha watu 3: mmoja ni msaili, msailiwa mmoja na mtazamaji mmoja. Kuwa msaili, unasaidia wanakikundi wenzako katika kupata picha ya wazi ya hali kwa kufuata hatua 5 za STARR. Wakati wa usaili unapoomba kazi, njia hii ya STARR hutumiwa mara nyingi sana. Kisha wasaili wanataka kusikia ushahidi fulani wa ujuzi wako na/au wanataka kutathmini kama una mtazamo mzuri wa kutafakari.'

**Utendaji**
1. Wagawe vijana katika makundi ya watu watatu.
2. Waulize vijana kufikiri na kuchagua tukio moja muhimu wakati wa wiki za mwisho za mafunzo ya viwandani. Inahitaji kuwa hali ambayo yeye alitumia uwezo wake, kipaji na ujuzi wake.
3. Eleza mbinu ya STARR. Ziandike herufi STARR zikiwa wima kwenye ubao na kuelezea mada tano (Hali, Jukumu, Shughuli, Matokeo na Tafakuri). Msaili A anamuuuliza maswali B juu ya mada 5. Kila mada ni hatua ya njia ya kupata picha ya wazi. Unaweza tu kuhamia kwenye hatua inayofuata wakati jibu linatolewa. Mwishoni mwa kila hatua, msaili hufupisha kile ambacho mtu B amesema.
4. Baada ya ufafanuzi wako, toa maswali kwenye karatasi ya zoezi namba 3.24 'STARR-njia ya kutoa maana ya uzoefu' na waalike kundi kutazama maswali kabla ya mahojiano kuanza.
5. Waelekeze vijana wafanye mgawanyiko kati ya mtu A, B na C. Mtu A kuanza kuuliza maswali kwa mtu B na mtu C anaandika yale yaliyosemwa. Waache waanze mahojiano.
6. Wakati mahojiano ya kwanza yamefanyika, tathmini kwa ufupi katika vipindi vitatu. Mtu B anaweza kutafakari juu ya kile alichojifunza kutokana na utaratibu wa kutazama nyuma ya kile kilichotokea. Mtu A atatafakari njia ya kuhojiana na mtu C anatoa maelezo yake juu ya washirika wote katika mahojiano na kukabidhi juu ya karatasi yenye maelezo yake kwa mtu B.
7. Baada ya tathmini fupi, badilisha majukumu kwa mahojiano ya pili. Kila mtu awajibike mara moja tu. Baada ya mzunguko wa pili, kuna mzunguko wa tatu.

**Tafakuri**
Ni kwa namna gani njia hii ilikuwa na manufaa kwa vijana? Je, wameona nini katika mazungumzo waliyokuwanayo? Je, wamejifunza zaidi kuhusu yao wenyewe? Kuna malengo mapya yaliyojitokeza kwa wakati ujao?


***Dondoo***
Si lazima 'kutatua' mambo yaliyotokea. Wazo la zoezi hili ni kutafakari zaidi juu ya uzoefu ambao ulikuwa muhimu na kujifunza kutokana na uzoefu huo, kuwapa maana na kuendelea. Kusisitiza kuwa ni muhimu kupata habari nyingi kadri iwezekanavyo. Kwa hiyo, msaili lazima afuate hatua 5. Waache waulize maswali wazi pia. Mpe mtu B, yule anayesema juu ya tukio hilo, muda wa kutosha kuelezea hali kwa ukweli kadri iwezekanavyo. Chunguza baadhi ya sababu kwanini muhtasari mwishoni mwa kila hatua ni muhimu.

**Uchunguzi wa kina**
Ili kuwasaidia vijana kutoa maana kwa uzoefu wao, ni jambo jema kufanya zoezi hili zaidi ya mara moja kwa mwaka. Kwa njia ya STARR, unaweza pia kufanya mazoezi ya usaili wa kuomba kazi. Katika somo la 6 unaweza kupata mazoezi zaidi ya suala hilo.

# KARATASI YA ZOEZI 3.1



Andika jina lako kwenye duara kubwa. Andika jina na taaluma za wanafamilia wote kwenye duara jingine. Kwa usawa uleule andika majina ya kaka na dada zako, juu yake andika majina ya wazazi wako, kaka na dada zao na juu kabisa babu na bibi yako. Kama familia yako ni kubwa zaidi ongeza matawi, maua au maduara zaidi.



# KARATASI YA ZOEZI 3.3

# MAANDALIZI YA KUMHOJI MTAALAMU

MADA YA 3.3

Usaili na (jina): ______________________

Taaluma: ______________________

Tarehe: ______________________

Wasaili:

a ______________________

b ______________________

c ______________________

Maswali tutakayouliza.

1 ______________________

______________________

2 ______________________

______________________

3 ______________________

______________________

4 ______________________

______________________

5 ______________________

______________________

6 ______________________

______________________

7 ______________________

______________________

8 ______________________

______________________

9 ______________________

______________________

10 ______________________

______________________

# KARATASI YA ZOEZI 3.5

Uzoefu wangu wa kazi ya malipo na isiyo ya malipo:

- 
- 
- 

Majukumu:

- 
- 
- 

Ujuzi, umahiri ambao nimepata wakati nafanya kazi hii:

- 
- 
- 

Mfanano na kazi ninayosomea:

- 
- 
- 



# UZOEFU WANGU WA KAZI MPAKA SASA

MADA YA 3.5

Utofauti na kazi ambayo ninasomea:

- 
- 
- 

Waajiri watategemea kwangu:

- 
- 
- 

Mategemeo yangu ya ziara ya kampuni:

- 
- 
- 

# KARATASI YA ZOEZI 3.6

**Ziara kwa:** ______________________________

**Jina:** ______________________________

**Anuani:** ______________________________

**Namba za simu:** ______________________________

**Jina la anwani yako:** ______________________________

**Tovuti:** ______________________________

- Haya ni maswali niliyonayo kwa kampuni

- Hiki ndicho ningependa kuona kwenye kampuni



# MATARAJIO YANGU KUHUSU ZIARA YA KAMPUNI

MADA YA 3.6

- Haya ndio maswali niliyo nayo kuhusu taaluma

- Hiki ndicho ningependa kuona kwenye kazi

- Hiki ndicho ningependa kufanya wakati wa ziara

# KARATASI YA ZOEZI 3.16

Kampuni: ____________________

Tarehe ya ziara: ____________________

Jina la msimamizi/mkufunzi wa kampuni: ____________________

- Kitu nilichopenda zaidi kwenye ziara hii ni:

  ____________________

  Kwa sababu: ____________________

  ____________________

  ____________________

- Sehemu hii ya ziara inatakiwa kuboreshwa:

  ____________________

  Kwa sababu: ____________________

  ____________________

# TATHMINI YA ZIARA KWENYE KAMPUNI

MADA YA 3.16

- Hiki ndio nilichojifunza katika ziara hii:

  ____________________

  ____________________

- Hiki nitakikumbuka daima kwenye ziara hii:

  ____________________

  ____________________

- Ninataka kumpa msimamizi/mkufunzi pongezi zifuatazo:

  ____________________

  ____________________

- Mwisho, ningependa kusema:

  ____________________

  ____________________

- Jina la mwanafunzi: ____________________

# KARATASI YA ZOEZI 3.24

**Hapa utakuta mifano ya maswali ambayo yanaweza kuulizwa utakapotumia mbinu ya STARR. Katika mbinu hii utatathmini hatua 5 kwenye vipengele vifuatavyo vya uzoefu: Hali, Jukumu, Utendaji, Matokeo na Tafakuri.**

**(STARR= Situation, Task, Activities, Result and Reflections)**

***Hali***

Inatueleza kuhusu kitu fulani-suala-ambalo limekuwa na faida wiki hii. Fafanua hali:

- Nini kilitokea?
- Lini na wapi kilitokea?
- Walihusika watu gani?
- Lilitokea wapi?
- Ulikuwa wapi?
- Watu wangapi walikuwepo?
- Ilikuwa namna gani?
- Lengo lilikuwa lipi?
- Ilikuwa saa ngapi?
- Ilichukua muda gani?

***Jukumu***

Elezea ungefanya nini katika hali hizi:

- Jukumu lako lilikuwa lipi?
- Ulitegemea nini toka kwako mwenyewe? Wengine walitegemea nini kwako?
- Nani alikupa jukumu hilo? Uliambiwa/uliagizwa kufanya hivyo?
- Ulikuwa na uwezo wa kumudu kazi hii?
- Ilikufaa?
- Ilionekana kuwa ngumu au rahisi kwako?
- Umeipenda?
- Nani walikuwa marafiki zako?
- Majukumu yako yaliishia wapi?
- Nani alikuwa kiongozi mkuu?



# STARR– NJIA YA KUTOA MAANA YA UZOEFU



***Utendaji***

Elezea namna ulivyoimudu hali:

- Katika hali ile ulionesha tabia zipi?
- Nini kilikuwa msaada na nini kilikuwa kigumu?
- Wateja na wenzako waliitikia vipi?
- Ulianzaje?
- Umeshafanya nini tangu?
- Kwanini namna hii?
- Ulijisikiaje wakati huo?
- Ulizuiaje hasira yako, kukatishwa tamaa, shauku n.k?
- Uliweza vipi kumaliza mjadala?
- Maneno yako hasa yalikuwa yapi?

***Matokeo***

Elezea nini kilikuwa matokeo ya mwisho ya kazi zako zote:

- Ni kigezo gani unatumia kufafanua matokeo chanya? Na matokeo hasi?
- Lilimalizika vipi?
- Uliridhika na namna lilivyoisha?

***Tafakuri***

Elezea unafikiria nini unapotazama nyuma wakati wa tukio:

- Nini kilifanyika kwa usahihi?
- Kwa mujibu wako, kipi kilitakiwa kufanyika kwa usahihi?
- Ungefanya nini wakati mwingine kwenye hali hii?
- Kuna kitu ambacho ungependelea kufanya kwa namna tofauti wakati mwingine?
- Una mawazo yapi sasa?
- Ungependa kujifunza nini siku zijazo?
- Unahitaji msaada gani? Kwa nani?